

# KUMKUMBUKA BWANA

 Asante. Bwana akubariki, ndugu. Nina furaha kuwa hapa, usiku wa leo, katika Southside Assemblies of God, kuabudu pamoja na nyinyi watu, tukiufurahia ushirika huu mzuri ambao hapana shaka mnaufurahia sikuzote.

<sup>2</sup> Nikiwa nimechoka tu kidogo. Tulikuwa huko chini jana usiku huko—huko Tucson, kwa ajili ya dhifa huko chini, na bila shaka tulikuwa na wa—wakati mzuri sana. Bwana alitubariki. Nami nimekuwa nikiishi juu ya ile sehemu yake nzuri, siku nzima.

<sup>3</sup> Kwa hiyo, sasa, nilikutana, nilimsikia mtu mmoja jana usiku. Kamwe sikumjua mwanawe Ndugu Carl Williams. Nilikuwa, leo hii, nikijivunia tu yule kijana mwanamume fulani aliyesimama na alikuwa akizungumza juu ya m—mkutano wa vijana. Nami nikamwambia binti yangu. Nikasema, “Sasa, unataka kuifanya hiyo shughuli yako kuingia kule.”

Akasema, “Simjui mtu yeyote mle.”

<sup>4</sup> Nikasema, “Utamjua mtu fulani, ama kila mtu atakujua. Ingia tu, haidhuru.”

<sup>5</sup> Nami ninaomba ya kwamba atapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kwenye mkutano huu huko juu.

<sup>6</sup> Nikasema, “Yule kijana mwanamume mzuri anayesimama pale, huku uso wake uking’ara kwa utukufu wa Mungu!” Nami nilikuwa nikilisimulia tena kwa Billy.

<sup>7</sup> Alisimama tu na kuniangalia, kasema, “Baba, hivi hujui huyo alikuwa ni nani?” Kasema, “Huyo alikuwa ni mwana wa Ndugu Carl Williams.”

<sup>8</sup> Vema, huyo, na—najua umetoka kwenye ukoo mzuri. Kama wewe... Unaona?

Nina furaha sana kuwa Phoenix usiku wa leo.

<sup>9</sup> Vema, kama hakuna Ndugu Pat Tyler. Ulitokea wapi, ndugu? Nadhani uliomba lifti, kutoka New York hapa. Hivyo karibu tu ndivyo mambo yaendavyo.

<sup>10</sup> Nakumbuka nikimwona Ndugu Gene, Ndugu Leo, hapa usiku wa leo, Ndugu Ed Daulton, wengi wa marafiki zangu hapa, na Ndugu Ed Hooper. Na, jamani, hapa juu usiku wa leo ninao mtazamo mzuri wa kila mtu, na ninaweza kuangalia huku na huku, vizuri.

<sup>11</sup> Vema, kidogo ninachoka. Nimekuwa nikifanya kazi sana, na kwa hiyo tuna—tuna saa nyingi. Na mimi... Mke wangu alisema, “Aisee, naona umeanza kuzungumza katika sauti yako ya pili.”

Nikasema, “Ilinibidi kuitumia wakati huu.”

<sup>12</sup> Wakati mwingine ninapozungumza, nashuka, nazungumza ndani kooni mwangu, ndipo sehemu hiyo inakuwa chungu na kuchoka. Ninapandisha, sehemu ya juu, ndipo nazungumza kutoka hapo, namna hiyo. Inatubidi tu kujifunza mambo ya kila namna tunapomfanyia tu Bwana kazi, sivyo, tunapochoka?

<sup>13</sup> Basi, jamani, ninatumaini kwamba hawa wote ni wahudumu hapa nyuma. Ikiwa ndivyo, jamani, tunatunzwa vizuri usiku wa leo, kundi zuri hivi la watu walioketi pamoja. Vema, hiyo inanikumbusha juu ya ahadi, kwamba, “Tunaketi pamoja mahali pa Mbinguni, Kristo Yesu,” ambapo Damu Yake hutusafisha na dhambi yote.

<sup>14</sup> Sasa nitajaribu, kwa kweli, kuwaacha mtoke mapema usiku wa leo. Tukikumbuka sasa kwamba, kesho usiku, tutakuwa kwa Ndugu Shores. Hilo ndilo jina lake? [Ndugu mmoja anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ndugu Shores, kwenye ya Kumi na Moja na Garfield. Hiyo ni Assembly of God nyingine huko nje. Naam. Assembly of God kule, na First Assembly of God.

<sup>15</sup> Halafu basi nitawasikiliza tu jamaa hawa wengine kwa muda mfupi sasa, mpaka Jumapili ijayo asubuhi, nadhani, kwenye ule mkutano. Mimi. . . Tutakuwa na wakati mzuri sana. Ninajisikia tu ya kwamba tutakuwa na wakati mzuri.

<sup>16</sup> Basi kusudi langu la kuwa hapa kidogo ni, loo, kidogo kutumika kwa niaba ya mwingine, mwajua, kuzunguka nikisaidia kila mahali, na ushirika mdogo pamoja na ndugu, na kuwa na usiku hapa na pale, kufahamiana. Na—na labda roho kidogo ya uamsho inaanza kuwashika watu, kisha kufanya utangulizi huo, yale tuwezayo, kuingia mle, halafu basi kwenye ule upeo mkuu. Nami nawazia, Ndugu Oral Roberts ndiye mtu wakati huu atakayeleta huo upeo kwenye dhifa Jumatatu ijayo usiku. Nami najua tunatarajia wakati mzuri sana, na kote katika juma.

<sup>17</sup> Kwa hiyo nyinyi mtuombee sasa, na mwende mitaani, mipakani na barabarani. Na ati “muwaombe”? La. “Muwashurutishe.” Muwashurutishe, muwashurutishe waingie. Kwa kuwa huu ungekuwa ni wakati mzuri sana kwa Phoenix kupata kuzuriwa kwake kukuu ambako nyinyi. . . Nami najua ya kwamba Mungu anapenda wakati tukiwa tayari, naam, bwana, tunapokuwa tayari. Hebu. . . Hiyo ndiyo sababu sisi. . . miamsho hii, ni kujaribu kukidhi hali za mambo, na kuomba sana, na kujitayarisha kwa ajili ya jambo hili kutokea.

<sup>18</sup> Sasa, kabla tu hatujalikaribia Neno, hebu na tuzungumze na Mwandishi, tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi. Sasa huku vichwa vyetu na mioyo ikiwa imeinamishwa kwa Mungu, nina hakika, katika kusanyiko la ukubwa huu, hapana shaka kuna haja nyingi. Na endapo una moja, nawe unataka kukumbukwa kwa Mungu, inua tu mkono wako, na nyuma ya huo, useme, “Bwana, unikumbuke.”

<sup>19</sup> Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unajua kilichoko nyuma ya kila mmoja wa mikono hii. Unajua ni kitu gani kilimulika niani mwao, na Wewe unaweza hata na zaidi kujibu kila haja. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia, Bwana. Tunaomba ya kwamba fadhila Zako zitatubariki, usiku wa leo, kwa njia ya kutumwagia Roho Mtakatifu juu yetu.

<sup>20</sup> Pia tukikumbuka, Bwana, ya kwamba, kesho usiku katika—katika First Assembly of God, ya kwamba Wewe utazimwaga baraka Zako tena juu yetu. Na halafu huko Ramada, kule kumalizia kwa juma hili, Ee Mungu, jalia moja kwa moja kuwe na mamia watakaokolewa. Tujalie, Bwana. Jalia kuwe na kumwagwa sa—sana kwa Roho hata magazeti hayawezi kutulia tena, bali itawalazimu kuutangazia umma yale yanayotendeka. Tujalie, Bwana.

<sup>21</sup> Jitambulisha tu Mwenyewe kwa watu Wako, Bwana. Jalia mioyo yao minyenyekevu ijitokeze kwa imani na kuamini ya kwamba tutayapokea mambo haya tunayoomba.

<sup>22</sup> Ndipo tutaomba, Bwana, kwa ajili ya wale ambao wangetaka kuwa hapa usiku wa leo na hawawezi kufika hapa. Hao ni wagonjwa na wanateseka, na—na katika hali ambazo wasingeweza kufika hapa. Tunawaombea, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu amzuru kila mmoja.

<sup>23</sup> Wabariki ndugu hawa ambao wamekuja kutoka mbali sana kupitia maeneo ya barafu. Na wengi wangali njiani, wakija. Walinde, Bwana. Waleta salama.

<sup>24</sup> Sasa, ibariki Assembly hii, mchungaji huyu mzuri, kusanyiko lake, wadhamini wake, mashemasi, na yote wanayosimamia, Bwana. Tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao na kuwasaidia. Sasa tunaomba ya kwamba Wewe utatupatia Neno Lako. Tunaweza tu kulisoma, Bwana, na kusoma fungu la maneno. Inabidi utupe muktadha, nasi tunakutazia Wewe. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>25</sup> Katika ki—kitabu cha Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11. Iwapo mtu fulani... Mwajua, kwa kawaida mnapenda kusoma, ama kuandika mahali, kusema, “Mimi...” Labda mtu fulani angepata kitu fulani nyuma yake ambacho labda wangeboresha yale yaliyokwisha kusemwa. Ama, wahudumu, na wakati mwingine walei, wanalichukua, na—na kulisoma tena, na kusikiliza yale yaliyosemwa. Mara nyingi mimi hufanya hivyo, ninaandika kifungu. Kwa hiyo kama mkitaka kusoma nyuma yetu usiku wa leo, fungueni Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, nasi tutaanza kusoma kwenye kifungu cha 23.

*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule... alitolewa alitwaa mkate:*

*Naye akisha kushukuru akaumega, akasema, Chukueni, mle: huu ndio mwili wangu uliovinjwa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Hiki ni kikombe cha agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*

26 Na sasa kwa ajili ya somo, ningetaka kuchukua kutoka hapo: *Kumkumbuka Bwana.*

27 Sasa, bila shaka, yeyote, sote tunajua, katika—katika kanisa letu, tunasoma hili kwenye ibada ya ushirika kila usiku. Na ni fu—fu—fungu zuri sana la maneno kusoma, ama Maandiko mazuri sana wakati huo, nayo yanatumika hapo. Lakini nilitaka tu maneno hayo, “Kwa ukumbusho Wangu.”

28 Sasa, ushirika mara nyingi umekuwa ni ubishi mkubwa kote katika nyakati, kati ya Protestanti na Katoliki. Wanasema Katoliki hula ushirika huu, nao wanaula katika matumaini ya kwamba wamefanya jambo fulani kustahili jambo jema, kwamba dhambi zao zitasamehewa kwa kufanya hivyo. Protestanti wanakula kama ukumbusho ya kwamba Kristo tayari amewasamehe, nao wanaula wakifurahi ya kwamba tayari wamesamehewa.

29 Paulo anaendelea kusema hapa ndani, ya kwamba—ya kwamba, jinsi ya kuikaribia meza ya Bwana. Kukiweko na kosa lolote, lisahihishe kabla hatujafika pale. “Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana.” Na sasa inatupasa kuwa katika maombi sana, sana tunapokula ushirika.

30 Lakini nimeshangaa mara nyingi ikiwa, neno hilo, tunalitumia vizuri tu, *ushirika*. Sasa, *shiriki* linamaanisha “kuzungumza na,” mnaona, “kushirikiana na.” Nami sijui kama kweli, tunapokusanyika pamoja namna hii katika mahali pa Mbinguni, kama huo si ushirika, kwamba tunashirikiana na Mungu, kuzungumza na Yeye.

31 Na, basi, laiti tungalikaa tu kimya na kumwacha Yeye atujibu! Mambo mengi, na moja ya mambo mabaya mno nifanyayo, mimi hujaribu kuzungumza pasipo ukomo, wala—wala siketi kimya muda mrefu kutosha Yeye apate kunijibu. Tunafanya hilo mara nyingi sana katika maombi. Nafikiri kama tungeondoa yale yaliyo moyoni mwetu, na kujieleza kwa Bwana Yesu, halafu tupige tu magoti, na tutulie tu kidogo na—na tuone tu yale Yeye angetujibu. Mnaona?

32 Na wakati mwingine nimefanya hivyo, ndipo maoni yangu yote yakabadilishwa, mnaona. Ningeenda na kumwomba Yeye kitu fulani, “Sasa, Bwana, watu hawa, kweli, wana kitu fulani. Na—naamini wananitaka mimi kule.” Nami ningeanza tu kuomba, na muda si muda mwajua, ni—ninaridhika tu ya

kwamba hayo ni mapenzi ya Bwana; lakini, baada ya kuomba, kama ni—nikitulia tu kidogo, mnaona, basi inabadilika, kabisa, wakati mwingine, ananituma mahali pengine. Zungumza tu na Bwana. Loo, ni ushirika mtukufu jinsi gani, kupiga tu magoti na kuzungumza, na kusemezana, na kumngojea Yeye ajibu.

<sup>33</sup> Na kuwazia ni Mtu mkuu jinsi gani ambaye unazungumza naye, Muumba Mwenyewe, na kusemezana na Yeye Yule aliyeweke uhai wako kwenye mavumbi haya ya volkano unamoishi. Ndipo basi siku moja itakubidi kuondoka hapo, ndipo basi liko mikononi Mwake liendako kutoka hapo na kuendelea. Nawe una majaliwa sasa kujichagulia ni wapi nafsi hiyo itakakokwenda hapo itakapoondoka.

<sup>34</sup> Na ni jambo zuri jinsi gani kufanya ushirika na Yeye juu ya msingi wa ahadi Zake, kisha kumsikia akikujibu, na kusema, “Yote ni salama.” Jamani, hilo—hilo kweli linalielezea vema. Haitubidi kuangalia kanuni yoyote ya imani. Haitubidi kuangalia fu—fundisho lolote la sharti. Jambo pekee litupasalo kufanya ni kujua tu ya kwamba Yeye hurejea na kulishuhudia Neno Lake, kwamba limetatuliwa, na ni hayo tu. Ndipo mzigo unabingirika na kuondoka.

<sup>35</sup> Nimewaza juu ya kuja kwenye meza hii, tunavyoiita usiku wa leo, sasa kwa vile nimelielezea ya kwamba huu hapa ni ushirika tu kadiri ya vile ingekuwa tukila kile tunachokiita chakula cha Bwana cha jioni.

<sup>36</sup> Mwajua, hao watu wa mashariki huko nyuma wamelivuruga kabisa jambo hilo, na—nami siwezi kuwanyosha juu ya hilo. Na huku kote kaskazini, wananichukua wakati nikienda kula chakula cha jioni, nao wanasema ni mlo mkubwa wa kutwa. Mimi—mimi... Wanasema ni kiamshakinywa, na chakula cha mchana, na—na—na—na chakula kikubwa cha kutwa. Sasa, chakula changu cha jioni kinaingilia wapi? Ninajaribu kuchunguza. Mnaona? Nao wanasema, “Loo, hayo ndiyo yote.”

<sup>37</sup> Nikasema, “Lakini haikuwa hivyo, hatukula mlo mkubwa wa kutwa wa Bwana. Yeye alikiita chakula cha jioni, chakula cha Bwana cha jioni.” Nami najisikia kana kwamba nimeruka mlo, kama mkikiita, mkianza kukiita hivyo.

<sup>38</sup> Lakini sasa tunapokuja pamoja namna hii, hapo Mungu hushuka. Nayo me—meza ya ushirika ni, kwa kweli, kumega, iliyomegwa, miili ya Mwili wa Bwana ambayo tunaigawa miongoni mwetu. Sasa, huo ni Mwili halisi, wa—wa mkate tunaoumega, ukiwakilisha Mwili wa Kristo.

<sup>39</sup> Hivi mliona katika Siku ya Pentekoste, ni jambo kubwa jinsi gani tulilo nalo pale? Ambapo, Mungu, Yule aliyewaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani, Yeye, ile Nguzo kuu ya Moto. Na kwenye Siku ya Pentekoste, Moto huu mkubwa ulishuka, kisha ukajigawa Wenye miongoni mwa watu Wake. Loo, kuwazia

jinsi ambavyo Yeye anatutaka kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, ndipo, kila mmoja akilifurahia joto hilo la Moto wa Roho Mtakatifu. “Ndimi zilizogawanyika zilikaa juu yao kama Moto, ndimi za Moto,” Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwa Kanisa. Loo, hilo, hata hivyo, si lingeiwasha tu moto mioyo yetu. Hapo ndipo tunapoweza kukusanyika pamoja katika mahali pa Mbinguni.

<sup>40</sup> Sasa, tunajua ya kwamba meza Yake, ambapo watu wanaketi pamoja na kufanya ushirika na Yeye, ni kama oasisi jangwani. Na oasisi, jangwani, ambapo pana chemchemi kuu, ambapo wasafiri waliochoka huja na kuketi kuizunguka oasisi hii jangwani, na—na kujiburudisha wenyewe, kisha kukumbuka jinsi ilivyofika pale.

<sup>41</sup> Na hivyo ndivyo ilivyo Kanisani, kwamba, meza hii ya ushirika ambapo baraka zote za Mungu, Injili yote, kila kitu alichopo nacho Mungu kwa ajili ya Kanisa Lake, kinatolewa, kinawekwa miongoni mwetu. Na ni kama o—oasisi katika jangwa hili lenye joto, linalowaka, lenye dhambi ambalo tunapitia. Ndipo basi tunapoingia, na kuzungumza juu ya, kusoma menyu, kisha tunaona ya kwamba Yeye anageuka tena, na Yeye si ndio kwanza atoke kwa *hii*, ama ndio kwanza atoke kwa *lile*, ama *hili* kufutuliwa mbali, bali Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yeye ana kila kitu kwenye menyu, tayari kukitoa. Hiyo ndiyo sehemu nzuri. Ndipo tunaweza tu kuangalia kwenye menyu na kuchukua tu yote. Mimi napenda tu. . . Ninapenda mlo mkamilifu. Nanyi je? Ninapenda tu kuula.

<sup>42</sup> Na wakati tukizifurahia baraka hizi, kila mmoja akiuhisi Uwepo Wake, na kusema, “Amina. Mungu asifiwe! Haleluya!” kadhalika, kwa kuwa tunaweza kukumbuka Yule aliyetuletea na kufanya iwezekane, mauti ya Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kumkumbuka Yeye. Nafikiri hivyo ndivyo, mara nyingi, kwamba labda tunafurahia baraka nyingi sana, hata tunasahau mahali zilipotoka.

<sup>43</sup> Wakati mmoja nilishangazwa sana. Nilienda na kundi la Wakristo wa kanisa fulani, nao wakaketi kula, wala hawakurudisha shukrani kwa Mungu, kwa ajili ya chakula chao. Vema, nilifikiri kidogo lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida. Kisha nikaenda kwenye nyumba nyingine, nao, bado, waliendelea na kula tu. Na mimi—mimi nikalihoji. Nao wakasema, “Loo, vema. Hiyo ni ninii tu. . . Mungu hutupa tu hicho, kwa vyovyote vile. Mnaona?”

<sup>44</sup> Nikasema, “Inanikumbusha juu ya nguruwe chini ya mtofaa, mwajua. Matofaa yataanguka, na kumpiga kichwani siku nzima; kamwe hataangalia juu, kuona yanakotoka.”

<sup>45</sup> Na hilo, mwajua, sisi, nafikiri inafaa kusimama na kuangalia juu, kuona ambako vitu hivi vinatoka. Loo, ni jambo la utukufu jinsi gani kumkumbuka Bwana wetu, kuyakumbuka

yote aliyotufanyia, na kukumbuka ya kwamba hapakuwapo na mwingine yeyote angaliweza kuliwezesha hili. Hakuna kitu kingaliliwezesha ila Bwana wetu. Na Yeye alilifanya bure, wakati hapakuwapo na mtu aliyestahili; hapakuwapo na nabii, hapakuwapo na mwenye hekima, hakuna kiongozi mkuu, hakuna mtawala, hakuna mfalme. Hakuna mtu angaliweza kulifanya ila Bwana Yesu, Mwenyewe, na Yeye alitufanyia hilo kwa hiari sana. Hebu tukumbuke tu. Yeye amewafanyia hilo watoto Wake kote katika wakati.

<sup>46</sup> Sasa hebu tuzungumze dakika chache tu juu ya jambo fulani ambalo inampasa mtu kukumbuka. Ningewazia, huko mbali sana Utukufuni usiku wa leo, kuna mtu jina lake Nuhu, naye hakika ana mengi ya kumkumbuka Bwana kwa ajili yake. Kwa kuwa katika wakati ambapo Mungu alitaka kuangamiza uovu wote kutoka kwenye uso wa dunia, Mungu alimkumbuka Nuhu. Naye Nuhu anakumbuka jinsi alivyoponea hasira ya Mungu, kwa rehema ya Mungu. Jinsi ambavyo ya—yale maji ya mafuriko yalianza kububujika mitaani, nazo pepo zikavuma, na miamba ikaondoka milimani! Basi ni tufani mbaya jinsi gani! Nyumba zikalipuliwa, nazo chemchemi zikapasuka, naye Mungu alikuwa amemweka Nuhu ndani ya safina. Sasa, kama hapo si mahali pa ajabu pa kumkumbuka Yeye, naam, naam, kuwa ndani ya safina, umewekwa salama katika Uwepo wa Mungu, kuishi pamoja na Yeye!

<sup>47</sup> Halafu tungeweza kuliita kundi lingine la watu, ama ningesema angalau watatu, nao waliitwa Shadraka, Mishaeli, na Abednego. Jinsi ambavyo walikuwa wamechukua msimamo wao kwa ajili ya Mungu, wakikumbuka ya kwamba Yeye hutimiza ahadi Yake! Na jinsi ambavyo, kwenye majira haya makuu, kwa sababu ya msimamo wao, hata ndugu zao wenyewe, wengi wao, walikuwa wamegeuka wakaingia ulimwenguni. Lakini wao watasimama, haidhuru, nao wakamtetea Mungu. Basi wakati tanuru lilipotiwa moto mara saba kuliko lilivyowahi kutiwa moto hapo awali, basi walitupwa kwenye tanuru hili.

<sup>48</sup> Nao hakika wanaweza kumkumbuka yule Mtu wa nne aliyekuwa mle ndani pamoja nao, aliyeweka jo—joto lote na mauti mbali nao. Kuna jambo fulani kuhusu huyo Mtu wa nne. Huenda tukazungumza juu Yake kidogo, naam, bwana, jinsi ambavyo Yeye alikuwa Ndiye pekee angaliweza kulifanya hilo liwezekane. Hapakuwapo na mtu mwingine angaliweza kulifanya ila huyo Mtu wa nne. Na ni Yeye Ndiye aliyetoa uhai, katika hatari ya mauti. Amina. Na Yeye—Yeye aliisukuma nyuma miali ya moto, na kuwahifadhi. Na, loo, mradi tu kunaweza kuwa na kumbukumbu, na hilo halitafifia, vivyo hivyo wanaweza kuikumbuka hiyo siku kuu huko chini Babeli.

<sup>49</sup> Kulikuwako na mtu mwingine kule chini Babeli, anayeweza kukumbuka pia, na huyo alikuwa ni Danieli, wakati alipoazimia

moyoni mwake kwamba hatajitia najisi kwa mambo ya ulimwengu.

<sup>50</sup> Huo ni msimamo mzuri kuchukua. Hapo ndipo sisi watu tunapaswa kuchukua, kidogo kuzikaza silaha zaidi kidogo. Jambo ndilo hilo. Hatutajitia najisi kwa mambo ya ulimwengu, haidhuru kanisa hilo lingine linafanya nini. Sisi wenyewe, tutajifunga silaha. Tutadumu moja kwa moja na hilo Neno.

<sup>51</sup> Haidhuru kijacho ama kiendacho, hatutajitia najisi. Kama hao wengine wanataka kufanya hivyo, endeeleni mkalifanye. Ikiwa hao wanawake wanataka kukata nywele zao, acheni wazikate. Sisi hatufanyi hivyo. Hiyo ni kweli. Kama wanataka kujipaka rangi za vidole, acheni waendele. Chochote kitu hicho kilicho, rangi, acheni waendele na kujipaka. Sisi hatutajipaka. Ikiwa hao wengine wanasema wanaweza kuvuta sigara na kuendelea, vema, acheni waendele. Bali sisi hatutafanya hivyo. Hivyo tu. A-ha. Hao wengine wanaweza kwenda nyumbani, waruhusiwe kuondoka kwenye shule ya Jumapili—Jumapili mapema, kwa ajili ya kipindi cha televisheni, ama Jumatano usiku, waache ibada yote kwa ajili ya kipindi fulani. Haijalishi wanafanya nini, sisi tutamtumikia Bwana.

<sup>52</sup> Tutachukua msimamo kama Yoshua, “Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana.” Tunakumbuka yale aliyofanya kutuletea baraka hii, nasi tunaifurahia sana hata hatuwezi kuitia najisi kwa njia yoyote. Ni hazina ya Uzima wa Milele tuliyo nayo, nasi kwa njia yoyote hatutaki kujitia najisi kwa mambo ya ulimwengu, hata kidogo.

<sup>53</sup> Naye Danieli aliazimu moyoni mwake jambo lile lile, ingawa alifanyika raia kule; bali si kwa chaguo lake, kwa sababu yeye alikuwa ni wa nchi nyingine. Na kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ni wa nchi nyingine mara tu anapozaliwa mara ya pili, kwa sababu anaelekea Mbinguni. Mali ya—yake iko Mbinguni.

<sup>54</sup> Basi hapa wakati fulani uliopita, mimi na mke wangu, karibu miaka miwili iliyopita, tulikuwa . . . Ndugu Mercier na hao wengine wataasisimkwa kidogo kutokana na hili, tuseme. Tulikuwa madukani. Basi katika mji wetu, ni . . . Loo, kunao watu wengi wa kidini, wanavyojiita. Lakini tuliona mwa—mwanamke aliyevaa sketi, nalo lilikuwa ni jambo la kigeni sana, maana hakuna mwingine wao aliyeonekana kuvaa moja. Na—na kwa hiyo tunajua wengi wao wanaoimba katika kwaya na kila kitu. Na ninii . . . na kwa hiyo sisi . . . Mke wangu akaniambia, akasema, “Vema, kwa nini?”

<sup>55</sup> Nami nikasema, “Vema, unaona, hao si—hao si wa uraia wetu.”

Akasema, “Ati nini?”

Nikasema, “La, hao si wa ninii wetu . . .”

Kasema, “Hao ni Wamarekani, sivyo?”

56 Nikasema, “Hakika. Hao ni Wamarekani. Hilo laweza likawa ni kweli vya kutosha.”

57 Ninakuta katika kusafiri, katika misheni, katika umishenari na kote ulimwenguni, nikienda U—Ujerumani, kuna roho ya kitaifa, inavyoitwa, ni roho ya Kijerumani. Ni roho ya taifa hilo. Nikienda Uswisi, ninakuta, ndugu tu, karibu wanazungumza lugha moja, bali kuna roho nyingine. Mnaona? Na ni roho tofauti huko Uswisi. Halafu ninakuja huku Ufini, ni roho tofauti kabisa. Ndipo ninakuja Marekani, kuna roho ya Marekani. Hiyo ni kweli.

58 “Vema, unasema, hivi sisi si . . .” Akasema, “Hivi sisi si raia wa Marekani? Ni kwa nini watu wetu, *hivi-na-hivi*?”

59 Nami nikasema, “Vema, unaona, mpenzi, unaona, kila taifa linaishi, kwa roho ya hilo taifa. Hiyo ni roho ya taifa.”

60 Akasema, “Vema, basi, hivi sisi si tungekuwa tukiishi kwa roho ya Marekani?”

61 Nikasema, “Loo, la.” Nikasema, “Tumezaliwa mara ya pili. Tunaishi kwa Roho ya Mbinguni, ambako kuna utakatifu, haki.”

62 Na sisi, sisi si Wamarekani, kwa jambo hilo, kwa sababu Marekani ni taifa tu la duniani. Lakini wakati mtu wa Ujerumani, wa Uswisi, ama popote awezapo kuwa, anapozaliwa kutoka Mbinguni, anachukua roho ya Mbinguni. Nayo tabia yake na maumbile yake yanatafuta vitu vya huko juu, ambako Kristo ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Amina. Loo, jinsi tunavyopaswa kukumbuka hilo, kwamba Yeye alikufa ili tuweze kukingwa na kitu hiki, kupata chanjo. Hiyo ni kweli.

63 Mmea mzuri wenye afya hauninii. . . Huna haja kuunyunyizia mmea mzuri wenye afya. Wadudu hawataushambulia, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli. Hakuna wadudu watakaousumbua mmea wenye afya. Ni ule wa namna ya tuta la kuoteshea ambao hauna budi kunyunyiziwa wakati wote, namna fulani ya mambo ya uhotara. Na hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Inatubidi kulinyunyizia na kulibembebeza kanisa mno. Inapaswa kuwa ni mtu mgumu wa Kristo, aliyeoshwa katika Damu ya Yesu Kristo, na kuzaliwa kwa Roho wa Mungu. Na wadudu wote wa ulimwenguni wanatawanyika. Hata hawajipumbazi karibu na pale, kwa vyovyote vile. Hilo ni fidhuli sana, bali natumaini lilishika. Kidogo ni tamshi fidhuli, bali mnajua yale ninayozungumzia.

64 Loo, jinsi ambavyo Danieli, akiazimia hilo moyoni mwake, anaweza kukumbuka vizuri faida yake. Nasi siku moja tutakumbuka faida yake, pia. Kwa hiyo wakati alipokuja kukumbuka hilo, katika saa ya dhiki, Mungu alimtuma Malaika kwenye tundu la simba, na kufunga kinywa cha simba, wasije wakamsumbua. Ni kumbukumbu la jinsi gani kuwazia! Yeye, alitupwa katika tundu la simba, kwa sababu alikuwa ameazimia moyoni mwake kumtumikia Mungu, naye angeweza kukumbuka

hilo. Iliendaje? Kitu kama hiki, “Mungu amemtuma Malaika Wake. Aliona uaminifu wa moyo wangu.” Loo, haya basi, usafi wa moyo wako. Mungu angeweza kuona hilo katika Danieli, na azimio lake kufanya yaliyo haki, ndipo Yeye akamtuma Malaika Wake na alikuwa amewazuia simba wasimsumbue hata kidogo. Ni kumbukumbu la jinsi gani! Tungeweza kuendelea na kuendelea, na hilo.

<sup>65</sup> Hebu tumkumbuke tu mtu mwingine mara moja hapa, ama kundi la watu, hao ni Israeli. Wakati Israeli walipokuwa wameweka mahali pao, kujiandaa wenyewe, kumtetea Mungu. Naye malaika wa mauti alikuwa akija usiku mmoja, aliyekuwa amchukue mzaliwa wa kwanza wa kila nyumba. Na jinsi ambavyo Israeli hata waliamriwa kukumbuka ya kwamba damu ilikuwa kwenye mwimo wa mlango. Hicho ndicho kitu kilichoizua ghadhabu ya Mungu, na kuwaweka pale, wakiwa hai, kilikuwa ni ile damu mlangoni. Ilikuwa ni ukumbusho. Na hiyo, daima, ingali ni ukumbusho, damu kwenye mwimo wa mlango na kwenye kizingiti. Ulikuwa ni usiku wa kumbukumbu jinsi gani! Nao ulikuwa ukaririwe kote katika nya—nyakati zijazo, ya kwamba Mungu, usiku huo, alitofautisha kati ya wenye haki na wasio haki.

<sup>66</sup> Loo, sijui kama ingekuwa ni kweli ama si kweli, bali siku yaja ambapo Mungu ataonyesha tofauti kati ya wenye haki na wasio haki. Nayo itakuwa ni ukumbusho kwetu, kujua ya kwamba ile Damu bila shaka iko kwenye kizingiti na mwimo wa mlango. Na popote unapoangalia, ama ufahamu wako; unaangalia kwa macho yako, na kuona kwa moyo wako. Hiyo ni kweli. Utakumbuka unaangalia kupitia Damu ya Bwana Yesu, jinsi ambavyo angeangalia kupitia kwake. Ni wakati wa jinsi gani! Walikuwa...

<sup>67</sup> Israeli walikuwa na jambo lingine waliloweza kukumbuka daima, kwamba wakati walipochukua hatua yao juu ya yale waliyosikia Musa akisema, yule nabii mkuu aliyethibitishwa kwa Neno la Mungu, basi wakati walipochukua msimamo wao kutembea taratibu. Kwa sababu, walimwona Mungu akithibitisha ya kwamba ujumbe aliokuwa akileta ulikuwa ni wa kweli, na ulikuwa ni kulingana na Maandiko, na Mungu alikuwa pamoja naye. Naye alikuwa amekutana na Huyu Ambaye hakuwa na jina, aliyetwa MIMI NIKO. Alikuwa amekutana na Yeye kweli, kwa sababu walikuwa wamemwona akitenda kazi na Musa.

<sup>68</sup> Na halafu walikuwa na ukumbusho mwingine mkuu, kwamba hapo walipoanza kutembea, Nguzo ya Moto iliwatangulia, kuwaongoza njiani. Ni kumbukumbu la jinsi gani wangeluweza kuwazia, jambo la ukumbusho, hata hawakuhitaji dira yoyote. Amina. Nilisema nini? Hawakuhitaji dira yoyote. Walikuwa na Nuru ya Mungu kuwaongoza.

<sup>69</sup> Ilikuwa ni ukumbusho wa jinsi gani kwa wale mamajusi, jinsi ambavyo hawakuhitaji dira yoyote, ndipo Nyota ikawaongoza.

<sup>70</sup> Ni ukumbusho wa jinsi gani kwetu leo hii, kuwa na Roho Mtakatifu kutuongoza; si kanuni fulani ya imani, au mtindo fulani, wala kitu fulani cha kutuongoza, au kitu fulani kilichobuniwa na mwanadamu. Lakini Roho Mtakatifu huja pamoja na nguzo ya kufungiwa ya Neno, na kulihakikisha Neno Lake, na kuthibitisha ya kwamba ni—ni kweli. Ni ukumbusho wa jinsi gani kwa mioyo yetu, kujua ya kwamba Mungu aliye hai angali hai. Loo!

<sup>71</sup> Kumkumbuka Yeye, yale aliyofanya, aliwaongoza kote hadi kwenye nchi ya ahadi, kwa njia hii.

<sup>72</sup> Eliya alikuwa na jambo kuu la kumkumbuka Mungu kwalo, akiisha kutekeleza jukumu lake, kile hasa Mungu alichomwambia afanye, kuamrisha mvua, hata umande usianguke mpaka auagize. Akakwea na kuketi karibu na kijito cha Kerithi, mle ndani. Akakaa huko wakati huu wote. Jinsi ambavyo angeweza kukumbuka hilo! Angepataje chakula, miaka hii yote? Lakini Mungu alimhudumia kwa kunguru. Mungu wa Mbinguni! Hakuna swali, “Kunguru hao walipata chakula hicho wapi?” Hatujui, hatuwezi kusema. Jambo pekee, kwamba alijua tu, alijikabidhi tu kwa Neno la Mungu, yale Yeye aliyomwahidi. Ndipo Mungu akashughulikia yaliyobaki.

<sup>73</sup> Hayo tu ndiyo yatupasayo kufanya. Ndugu, hayo tu ndiyo tunayohitaji. Ni kumchukulia tu kwa Neno Lake. Atafanyaje jambo hilo? Sijui. Lakini, mnaona, tunajaribu kuingiza mawazo yetu wenyewe, na hapo ndipo tunapovuruga mambo.

<sup>74</sup> Vipi kama angalisema, “Kijito hiki kingine chini ya kilima kingekuwa kizuri vile vile, maana kina maji mengi zaidi”? A—ha. La.

<sup>75</sup> Vipi kama Ibrahimu angaliwazia ya kwamba anapaswa kuiteka Sodoma? Kamwe lisingalitendeka vizuri. Bali Ibrahimu alipitia njia ile aliyooongozwa na Bwana, ile ahadi yake moja aliyopaswa kushikilia.

<sup>76</sup> Eliya angeweza kukumbuka wakati alipokuwa amefanya yote aliyoweza kufanya. A—alikuwa amewakemea wa—wanawake wote wa siku hiyo, waliojaribu kujifanisha na mama taifa, mke wa rais, na—na mambo hayo yote ambayo a—alikuwa ameyakemea. Na—nao wakamwita mzee, nadhani, jamaa mzee tu, duni. Naye akaenda, ila akafanya yale hasa Mungu aliyomwambia afanye. Ndipo ikafikia kwenye mashindano ya kuamua, ambapo yeye alisema, “Hebu tuone ni yapi, ya mambo haya, yaliyo kweli. Sasa, nyinyi waiteni manabii wa—wa Baalimu hapa juu, na—nanyi muwaite manabii wake. Nami acheni nimwite Bwana.” Loo, ni shindano la kuamua la jinsi gani, wakati alipojua Neno Lake lilikuwa limeliahidi.

<sup>77</sup> Tungesema nini leo hii kama Wakristo, mbele ya Ubudha, Uislamu, ama chochote kingine? “Hebu tuone nani ndiye Mungu.” Amina.

<sup>78</sup> Wakati fulani uliopita, chini huko India, ambako tulikuwa kwenye—kwenye mkutano, nako kulikuwako na watu wengi, lakini wanne ama watano wakaja jukwaani. Na hapakuwapo na njia ya kukadiria ni watu wangapi waliokuwa pale. Ndipo nikamwombea maskini mtu mwenye ukoma. Hakuwa na mikono, na masikio yake yalikuwa yameliwa yote, na vigutu vidogo tu. Naye alikuwa akijaribu kunikumbatia, nami nikamkumbatia, na kuomba pamoja naye. Bwana akaniambia kilichokuwa shida yake, na—na kuhusu maisha yake.

<sup>79</sup> Na—nami ningeweza kuwaona Maraja na hao walioketi pale nje. Wakasema, “Hiyo ni telepathia, mnaona.” Ungeweza—ungeweza kujua, vile walivyokuwa wakiwazia, kile walichokuwa—kile walichokuwa wanaenda kunirudishia.

<sup>80</sup> Siku hiyo, nilikuwa nimekaribishwa katika hekalu la Majaini, ambapo palikuwapo na yapata dini kumi na saba mbalimbali mle ndani, na kila moja ya hizo inaupinga Ukristo, na, “Ukristo ni bure.”

<sup>81</sup> Lakini, usiku huo, Mungu akabadilisha ratiba. Tukaanza kusoma kutoka kwenye menyu, karibu na chemchemi Yake. Kwa hiyo Roho Mtakatifu akaanza kufunua. Na baada ya kitambo kidogo, Mhindi mmoja akaja karibu, naye alikuwa ni kipofu. Nikasema, “Mtu huyu ni kipofu. Sote tunaweza kuona hilo. Bali ni mtu aliyeoa. Anao wana wawili.” Nikasema, “Nitataja herufi za jina lao. Si—siwezi kulitamka.” Na hiyo ilikuwa ni kweli kabisa. Ni—ningeweza.

<sup>82</sup> Hao wanaowaita watu watakatifu, na hao wote huko nje, na hao makasisi wa Kiislamu, nao wameketi pale nje. Na kwa hiyo wa—walijua basi, walidhani nilikuwa nikisoma nia zao, telepathia.

<sup>83</sup> Na kwa hiyo ilitokea kwamba nilianguka nyuma, naye mtu huyu kipofu, ono tu hapo juu, alikuwa amesimama pale akiniangalia. Loo, jamani! Mwajua, Mtumishi wa Mungu, Roho Mtakatifu, alikuwa tayari ameleta... yale yaliyoandikwa kwenye menyu, mwajua. Nilijua kilikuwa tayari kupakuliwa.

<sup>84</sup> Nikasema, “Sasa, walikuwa wakiniambia leo hii ya kwamba dini ya Kiislamu ndiyo iliyo kuu kuliko zote ulimwenguni, na Wabudha, na zote.” Nikasema, “Sasa, ninataka baadhi yenu makasisi huko nje, makasisi wa Budha, makasisi wa Kiislamu, waje wayafungue macho ya mtu huyu, hakika, sasa, kama yeye—yeye ni mkuu hivi. Mtu huyu ni mwabudu jua. Nasi sote tunajua, sisi tunaoamini ya kwamba alikosea, aliabudu kiumbe badala ya Muumba.” Nikasema, “Alikosea, nasi tunajua hilo. Lakini,” nikasema, “hakika Mungu aliye Muumba; naye mtu huyu yuko

tayari kuja na kumtumikia Muumba huyo; hakika Yeye yuko tayari kujidhihirisha Mwenyewe.”

<sup>85</sup> Sasa, ninataka kusema jambo fulani. Nisingalisema hilo kwa vyovyote vile kama sikuwa nimeliona ono hilo. Nilijua vema kuliko hivyo. Mnaona, hilo ndilo hatutaki, kwenda tukidhania. *Kudhania* linamaanisha “unapiga hatua pasipo na uhakika.” Hiyo ndiyo sababu tunataka kuwa waangalifu unaposema BWANA ASEMA HIVI, sio tu dhana, lakini kitu unachojua kwa hakika, kikweli, Bwana amekisema. Nami nikajisikia kufarijika sana kwa kuliona hilo ono, nikijua halijawahi kushindwa.

<sup>86</sup> Ndipo nikasema, “Sasa, ninii—ninii... Kama mtu huyu amekosea... Sasa, Waislamu wanasema alikuwa amekosea, halafu ninyi kumfanya Mwi—Mwi—Mwislamu. Halafu, Wabudha wangesema alikuwa amekosea. Nao Makalasinga, na Wajaini, na wowote wale, wote wangesema amekosea. Lakini hakika kuna Ukweli mahali fulani.” Loo, jamani! Loo, ni kitu chenye utukufu jinsi gani! Ndipo nikasema, “Sasa, Yule atakayefungua macho yake, yeye aliahidi atamtumikia Mungu huyo.”

<sup>87</sup> Aliingia upofu, kutokana na kulitazama jua, maana lilikuwa ni mungu jua. Mnaona? Naye alidhania hilo liliilipia safari yake ya kwenda Mbinguni. Sasa, tungeweza kumkumbuka Kristo, ya kwamba Yeye—Yeye aliteseka sio apate kuyapofusha macho yetu, bali kuyafungua macho yetu. Mnaona? Kwa hiyo basi, na ikiwa...

<sup>88</sup> Nikasema, “Sasa, Yule atakayekuja na kufanya jambo hili, nitalifuata kundi hilo la dini.” Nikasema, “Nitamtumikia Yeye atakayefungua macho yake.” Basi hilo lilikuwa ndilo kundi nyamavu kuliko yote nililopata kusikia. Hakuna mtu aliyenena. Ndipo nikasema, “Vema, huyo hapo kasisi wa Kiislamu hapo nje sasa, mbona usije ukayafungue macho yake?” Nikasema, “Kwa nini? Ni kwa sababu huwezi. Na wala mimi siwezi. Bali Mungu wa Mbinguni amemfufua Mwana Wake, Yesu Kristo, Ambaye amenionyesha ono sasa hivi, ya kwamba huyu mtu atafumbuliwa macho yake. Ikiwa sivyo, basi mimi ni shahidi wa uongo wa huyu Kristo. Na kama akifanya hivyo, basi mimi ni shahidi Wake wa kweli. Nanyi inawabidi ku... Mnapaswa kutubu, ama hamna budi, kama ninyi... la sivyo mtaangamia katika makundi ya dini mliyomo sasa.” Ni wakati wa jinsi gani! Basi nikasema, “Sasa, iwapo huo ni uongo, basi mnapaswa kuniweka kwenye ndege mkanirudishe Marekani, wala msiniruhusu kuingia humu tena.”

<sup>89</sup> Loo, lakini hapo Mungu wetu alipojitokeza jukwaani! Huyu mtu, mara nilipomwombea, aliweza kuona vizuri kama nilivyoweza. Alikimbia akamrukia meya wa mji shingoni na akaanza kumkumbatia. Na, mbona, tulichukua kama saa nne. Sikuwa na viatu, wala mifuko ya koti langu, na jeshi la

mgambo lisingeweza kuwazuia, na ilikuwa ni mkurupuko. Nanyi inawapasa kuona kile. . .

<sup>90</sup> Lakini ilikuwa ni kitu gani? Mungu yule yule, Mungu yule yule aliyeweza kuagiza moto, kushusha moto, kuiondoa dhabihu Yake; anaweza kumleta Roho Wake Mtakatifu, kuthibitisha Neno Lake, kwamba ni Kweli, mradi tu una hakika kwamba hiyo ni Kweli.

<sup>91</sup> Sasa, Eliya alikuwa na hakika ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. Alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu. Hakuna swali kwake.

<sup>92</sup> Wala hakuna swali moyoni mwako usiku wa leo, ya kwamba Mungu angali anatoa Roho Mtakatifu kama alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, litatukia. Ikiwa hakuna swali kwamba Yeye hutimiza Neno Lake na kuwaponya wagonjwa, halina budi kutukia. Lakini huna budi kuwa na hakika nalo. Huna budi kuliona kweli kwa macho halisi ya imani, kisha ulikubali na kusimama papo hapo.

<sup>93</sup> Naye alikuwa na mengi sana ya kumkumbuka Mungu kwa ajili yake, hapo alipokuwa. . . Sasa yeye ana mengi ya kukumbuka, yale Yeye aliyofanya katika siku hizo.

<sup>94</sup> Yule mwanamke mtovu wa uadilifu ambaye Yesu alikutana naye huko juu Sikari, kwamba yeye alikuwa ni Msamaria, ambao walikuwa ni watu waliotengwa na jamii ambao walimwamini Mungu kweli. Walikuwa kama nusu Myahudi na nusu Mmataifa, nao walikuwa ni ja—jamii. Walimwamini Mungu. Na maskini mwanamke huyu, mtovu wa uadilifu katika hali yake, amechafuliwa sana na dhambi, basi siku moja labda alivunjwa moyo na mapokeo yao yote ya wazee, ya vyungu na mabirika, na kuosha, na kadhalika.

<sup>95</sup> Alitoka akaenda siku moja kwa maskini kisima kile cha kale cha Yakobo kule juu, naye alikuwa akitaka kuitelemsha ndoo ya—yake, akachote maji. Ndipo akabadilisha chemchemi. Loo, jinsi anavyoweza kukumbuka ya kwamba kulikuwako na Mtu aliyeketi pale ambaye alisema, “Ndani Yake mlikuwamo na Maji yaliyo hai.” Jinsi lilivyomchangamsha, wakati Kisima hicho hai kilipozifichua dhambi zake, na kumwambia mahali alipokosea, na kumwelezea yale aliyokuwa amemfanyia. Nalo likaweka ujumbe moyoni mwake, uliompasha moto kwa utukufu wa Mungu; na huyo akaingia mjini, na kwa hao wanaume.

<sup>96</sup> Sasa, mwajua, hilo kweli si halali katika nchi hiyo, kwa mwanamke kupitia mitaani, na hasa mwanamke aliyetiwa alama kwa utovu wa uadilifu. Lakini nawaambieni, hapo aliposafishwa na kunyweshwa Maji hayo matamu, ati ujaribu kumzuia? Ilikuwa ni kama kujaribu—kujaribu kuuzima mo—moto, ama nyumba inayoteketea, na ni kukavu sana, na upepo mkali katika hali kavu, uliokuwa ukiuvumisha mwali moto huo kwelikweli.

<sup>97</sup> Wala usingeweza kumkomesha, kwa sababu alikuwa amepata kitu kilicho halisi. Dhambi zake zilifunuliwa.

Basi dhambi zake na makosa yalipofunuliwa, yeye anaweza kukumbuka usiku wa leo, Utukufuni. Anaweza kukumbuka ya kwamba kulikuwako na Chemchemi kwa ajili yake. Kulikuwako na mahali ambapo, kanuni zote za imani na—na makanisa yalikuwa yememkataa, bali hata hivyo alipata oasisi. Alipata mahali ambapo kuna Mtu Ambaye alijali. Ni shangwe jinsi gani!

<sup>98</sup> Na jinsi tunavyoweza kushangilia pamoja naye, sisi ambao tulifungwa na kanuni za imani zilizotuvuta mbali na Mungu, na tukapata Chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli. Hapo tulipoteza hali yetu yote ya ugumu. Ndipo—ndipo tukainywea hiyo Chemchemi na kuburudika. Pia tunakumbuka Yule aliyeilipia gharama, tupate kuwa na Roho Wake juu yetu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Ni ukumbusho wa jinsi gani kuukumbuka!

<sup>99</sup> Ninawazia usiku wa leo ya kwamba Hajiri angeweza kuwa na jambo la kuwazia, pia, wakati alipokuwa amefukuzwa, kueleweka vibaya. Sasa wapo wengi wetu hapa wanaoweza kuwazia juu ya Hajiri, jinsi yeye, akieleweka vibaya.

<sup>100</sup> Ni nani atembeaye maisha mema pamoja na Mungu, ambaye huipitia ile njia nyofu, nyembamba, ila anayejua kueleweka vibaya ni nini? Mimi nimeeleweka vibaya. Kila mtu, ninyi nyote ndugu mnaojaribu kuishi vema, nanyi kina dada, mnaeleweka vibaya.

<sup>101</sup> Jirani zako wanafikiri wewe ni mtindo fulani wa kale, nao wanajaribu kukushambulia. “Kwa nini huhudhuri mashirika haya? Na ni kwa nini hufanyi karamu hizi za kadi, wakati mambo?” Nawe unayakwepa mambo hayo. Unaeleweka vibaya.

<sup>102</sup> Vivyo hivyo Hajiri alieleweka vibaya. Naye alikuwa na mtoto wake, maskini Ishmaeli, aliyekuwa ni tunda la tumbo lake, kutoka kwenye ndoa halali na mume wake Ibrahimu. Naye alikuwa—alikuwa msichana mtumwa. Naye alikuwa amekabidhiwa na bimbubwa wake, Sara, kwa Ibrahimu, amwoe; ambapo, ndoa ya wake wengi ilikuwa halali siku hizo. Naye alikuwa ameolewa kihalali na huyo mtu, kwa sababu alikuwa amekabidhiwa kwake. Alikuwa amemzaa mtoto, kile tu kilichokuwa matumaini yao. Hakuna kitu ambacho mwanamke huyo alikuwa amefanya kinyume. Na, hata hivyo, alieleweka vibaya na bimbubwa wake, na kufukuzwa aingie nyikani apate kufa. Ni mahali pa jinsi gani kuwa!

<sup>103</sup> Nayo maji yalikuwa yamekwisha kwenye chupa. Koo la maskini Ishmaeli lilikuwa limeanza kukauka. Alikuwa akilia apate maji. Ikafikia pabaya zaidi. Basi ni moyo wa mama pekee ungaliweza kumsikia mtoto huyo akilia kutoka kwa midomo midogo iliyokauka, ja—jangwani mahali fulani, ya mtoto wake wa pekee, na kuhisi maskini mwili wake ukikauka, naye yuafa. Hakuna maji, ni mawe tu na mchanga, kama vile ungetazama

nje hapa katika majangwa ya Phoenix. Sio mahali. Kueleweka vibaya! Ni wakati wa jinsi gani!

<sup>104</sup> Alikuwa ndiye huyo hapo, msichana mtumwa, kwanza, naye alikuwa amejaribu kutenda kwa njia sahihi aliyopaswa kutenda. Naye huyu hapa ana mtoto mchanga mikononi mwake, naye yuafa. Basi alikuwa na huzuni sana. Akamlaza chini ya kichaka kidogo. Kisha akaenda kadiri ya mtupo wa mshale, akapiga magoti kuomba. Ndipo kisima kikaonekana, loo, jamani, “Kisima cha Yeye aliye hai na anayeniona.” Kingali kipo hata leo. Kiliwekwa pale, kwa njia fulani. Kisima hicho kingali kinasimama kama kumbukumbu.

<sup>105</sup> Sina elimu ya kutosha kulitamka. Lakini ni—nililijaribu, muda mfupi uliopita, nilipokuwa nikiandika muhtasari kidogo. Nami ni—nikajaribu kulitamka. Nisingeweza kulitamka. Lakini mnajua ni nini. Ni—ninakiita kitu kimoja, kingine. Nikasema, “Afadhali nisiseme hilo. Litaonyesha tu ujinga wangu vibaya zaidi.”

<sup>106</sup> Ila jambo moja ninalotaka kusema. Ninajua mahali palipo na Kisima kingine kilichowekwa kwenye Siku ya Pentekoste. Ki wazi tu usiku wa leo kama kilivyokuwa wakati kilipofunguliwa huko nyuma, nayo maji hayo ni matamu tu vile vile kwa kila mwanamume au mwanamke anayetaka kupitia barabara ya kweli pamoja na Neno la Mungu, na kutembea pamoja na Yeye.

<sup>107</sup> Naja kwenye kisima hiki, nikimkumbuka Yesu aliyefanya iwezekane kwamba mimi, mgeni, mwana wa mlevi, ningeweza kuja kwenye Kisima hicho na kusamehewa dhambi zangu, na kuunywea Uzima wa Milele.

<sup>108</sup> Loo, jinsi hapana shaka Hajiri alijisikia wakati alipoona kisima hicho! Kiliyaokoa maisha yake na ya mtoto wake. Hakika anaweza kuikumbuka oasisi hiyo, siku zote za maisha yake, na kote—kote kupitia wakati ambapo anaweza kuikumbuka.

<sup>109</sup> Tungeweza kuendelea na kuendelea, na watu. Lakini, hebu tuliwazie tu hili, usikose kukiona kisima chako sasa. Usikose kuona ile sehemu ya kuburudisha inayoleta Uzima.

<sup>110</sup> Yesu alitumwa kutoka kwa Herode kuninii. . . kutoka kwa Pilato hadi kwa Herode, kwa ajili ya dhihaka. Kile alichokosa! Ni nini, ni nini iliyokuwa shida ya Pilato?

<sup>111</sup> Basi hapo Pilato alipomtuma Yesu kwa Herode, halafu basi jinsi Herode alivyokuwa mpumbavu. Ambapo, alikuwa amesikia habari Zake, pia alikuwa amesikia habari za huduma Yake. Naye Pilato akiwa ni Myahudi. . . Ama, Herode, ninaamini alikuwa, Herode alikuwa ni Myahudi. Huku amesimama pale mbele Yake! Basi huyo hapo, amesimama Mbele ya yale manabii wote walikuwa wametabiri kuhusu, tangu Edeni na kuendelea. Amesimama katika Uwepo, na kamwe hakuomba msamaha wa dhambi zake. Yeye kamwe—yeye kamwe—yeye kamwe. . . Nashangaa kama hata aliwazia, alichukua wazo la pili, ya kile,

kwamba alikuwa amesimama mbele ya Nani? Labda hakujua kamwe ni Nani—Nani alikuwa amesimama Mbele zake.

112 Loo, mnasema, “Hilo lilikuwa—hilo lilikuwa tishio! Hilo lilikuwa ndilo jambo la kijinga kuliko vyote.” Lilikuwa. Lilikuwa ndilo jambo la kijinga kuliko vyote ambalo mtu huyo aliwahi kufanya. Vema, tunawazia juu ya—juu ya vile alivyokuwa katika hali mbaya.

113 Lakini ngoja kidogo. Tunao watu siku hizi wanaofanya jambo lile lile, wanasimama karibu na Chemchemi ile ile, na wangali wanafanya kosa lile lile alilofanya.

114 Manabii wote, kwa miaka elfu nne walikuwa wameelekeza Kwake. Lakini kwa sababu hakuja katika njia ya kanuni zao za imani, zilivyosema Yeye angekuja, walimtupa nje.

115 Hapo, ni kweli kabisa. Ni kweli kabisa. Naam, bwana. Wangali wanamtupa nje. Hawataki uhusiano wowote nalo, isipokuwa lije kulingana na kitabu chao, mwajua, jinsi ambavyo kitabu chao cha kiada kinavyolisema, mnaona. Halina budi kuja hivyo.

116 Loo, manabii wote kupitia miaka elfu nne walikuwa wamenena habari Zake, naye Huyu hapa amesimama mbele zake, wala hakusema kitu kuhusu, kuomba msamaha. Huyu hapo katika huo Uwepo, na u—utimilifu wa maneno yote ya manabii wa Kiebrania, amesimama papo hapo mbele yake, na hata hakuomba msamaha. Alisimama tu pale. Loo, hilo lilikuwa ni jambo la kuchukiza mno!

117 Lakini tunafanya jambo lile lile siku hizi. Ila tu, tunasimama karibu na Yeye, baada ya miaka elfu sita. Tunafanya kosa kubwa zaidi kuliko Herode, na Pilato, na—na Kayafa, na makuhani wa siku hiyo, kwa sababu tuna miaka elfu mbili zaidi ya kumbukumbu iliyoongezewa. Nasi tungali tunafanya kosa lile lile. Ninii tu, ninaninii tu. . .

118 Nadhani ya kwamba—ya kwamba Herode kamwe hakuliwazia kwa uzito.

119 Sasa, sijui tu jinsi tunavyoliwazia Hili kwa uzito. Unajaribu kulitafakari Neno hili kwa uzito kiasi gani? Neno hilo linamaanisha nini kwako? Unajua huyo ni Mungu katika maandishi? Bali tunapita moja kwa moja juu yake, kwa ajili ya namna fulani ya kanuni ya imani, na kusema, “Siku za miujiza zimepita. Dk. Jones alisema *hivi-na-hivi*, kwa hiyo hilo latosha.” Na, hata hivyo, Biblia hii imewekwa katika kila duka la vitabu, karibu kila kimoja, kibanda cha Biblia, makanisani. Nao wahudumu, na kadhalika, wamesimama pale, nao wanasoma kupitia juu yake, na kuipuuza, kwa ajili ya kanuni ya imani, wanajaribu kuiweka huko nyuma katika kipindi kingine cha wakati.

<sup>120</sup> Kama vile nilivyotoa tamshi, mara mbili ama tatu tangu niwe huku Phoenix, lilinjia. Wanadamu wako hivyo. Daima wanamsifu Mungu kwa ajili ya yale Yeye amefanya, na kutazamia yale atakayofanya, huku wakipuuza yale anayofanya sasa hivi. Wanafanya hivyo. Wanakosa kuliona.

<sup>121</sup> Sasa, labda Herode angaliweza kumsifu Mungu kwa ajili ya vile alivyowatoa watoto kutoka nyikani, na kadhalika. Nao wakasema, “Siku moja Yeye atamtuma Masihi. Utukufu kwa Mungu! Tutamwona wakati huo.” Naye alikuwa Huyu hapa, amesimama moja kwa moja mbele yao, nao hawakumjua.

<sup>122</sup> “Alikuwako ulimwenguni, nao ulimwengu uliumbwa na Yeye, nao ulimwengu haukumtambua. Bali wote waliompokea, kwake... aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu.” Ninapenda hilo. Naam, bwana.

<sup>123</sup> Hapo katika Uwepo Wake, nadhani hakuliwazia kwa uzito.

<sup>124</sup> Na wengi siku hizi wanafanya jambo lile lile, hawalitili maanani. Hawaliwazii kwa uzito. Wanawazia, “Sasa hapa, mimi huenda kanisani, nami ni mzuri tu kama ulivyo wewe.”

<sup>125</sup> Sasa, kamwe hutaki kuchukua msimamo huo. Ungeweza kuwa mzuri kama mimi, na usiwe mzuri hata kidogo. Unaona? Lakini unapaswa kutomfanya mtu yeyote mfano wako. Unataka kumfanya Mungu Mfano wako, Yesu Kristo, nawe unataka kuchukua Neno Lake. Basi kama huninii...

<sup>126</sup> Sasa, kumbukeni, Biblia ilisema, huku katika kitabu cha Ufunuo. Huu ndio ufunuo kamili wa Yesu Kristo. “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, au kuliweka neno moja Kwake, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.” Kwa hiyo Huo ndio Ufunuo.

<sup>127</sup> “Mungu zamani za kale na kwa njia mbalimbali,” Waebrania 1, “alisema na baba zetu kupitia manabii, lakini siku hizi za mwisho kwa Mwana Wake, Kristo Yesu.” Na, Kristo, akijifunua Mwenyewe, akijitambulisha Mwenyewe, akilichukua Neno Lake na kulifanya tu listawi.

<sup>128</sup> Nikisimama hivi majuzi, nikizungumza, ninaamini, na Ndugu Carl Williams, palikuwapo na mtende. Ninaamini ilikuwa ni Ndugu Carl, ama mtu fulani. Ndipo nikasema, “Huo si ni mti wa kupendeza?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Ni kitu gani? Mavumbi ya volkano.”

<sup>129</sup> Hivyo ndivyo tu ulivyo, mavumbi ya ardhini, yenye uhai ndani yake. Na uhai huo ulikuwa ni uhai wa namna fulani, uliufanya mtende. Hapa unasimama mwingine, ni mti wa namna nyingine. Ni mtini. Ni kitu gani? Mavumbi ya volkano kutoka ardhini, yakiwa na uhai wa mtini ndani yake.

<sup>130</sup> Vema, tuangalie sisi. Sisi ni nini? Ni kama mti ule, mavumbi ya volkano, bali yakiwa na uhai wa binadamu ndani yake. Nao uhai huo wa binadamu ni wa ardhini, na hauna budi kurudi ardhini.

<sup>131</sup> Lakini kuna Uzima utokao Juu, ambao, mwanadamu, yeye huishi kwa Uzima huo. Ni Uzima wa Milele.

Ni upumbavu jinsi gani! Hivi hatungeweza kutafakari hayo, enyi marafiki?

<sup>132</sup> Sasa, si mhemuko. Sio kuweka kanuni nyingi za imani. Ni tukio. Ni Kuzaliwa. Kwanza, inakubidi kuwa na ujuzi wa mauti kabla ya kuweza kushuhudia Kuzaliwa. Kama vile, kulinyosha hilo vizuri: onja mauti, kisha ushuhudie Kuzaliwa. Mbegu yoyote haina budi kufanya vivyo hivyo. Nayo Mbegu *hii* ni Mungu. Na wakati Hiyo imewekwa moyoni mwako, inasababisha Kuzaliwa kwa mwana wa Mungu.

<sup>133</sup> Na hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa wakati alipokuwa duniani. Alisema, “Ni nani awezaye kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi? Ni nani anayeweza kunishtaki Mimi, hasa, kwamba nina dhambi?” *Dhambi* ni “kutokuamini.” “Kama—kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi.” “Yachunguzeni Maandiko. Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Hayo Ndiyo yanayosema Mimi ni Nani. Basi ikiwa Mimi sitimizi sifa hiyo, jinsi hasa Maandiko yalivyosema, Baba alivyosema ngingekuwa, hapo nitakapokuja; kama sitimizi hayo, basi nimekosea.”

<sup>134</sup> Loo, kama sisi Wakristo, kama sisi wahudumu, kama sisi wanaume, wanawake, Wapentekoste, na wengine wetu, kama hatuwezi kuyachukua yale Mungu aliyosema kanisa Lake linapaswa kuwa, kama hatuwezi kulingana na kiwango hicho alichosema, basi tunaweza kuhukumiwa kwamba tuna dhambi, ya kutokuamini. Tunajaribu kusema ya kwamba siku za miujiza zimepita, na mambo haya mengine yote, *hayo*, na *hili-na-hili*, na *hili-na-hili*, ndipo tunaweza kushtakiwa kwa kutokuamini. Kwa kuwa, ipo dhambi moja tu, na hiyo ni kutokuamini. “Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari.” Mnaona? Hata hufikii msingi wa kwanza ikiwa huamini. “Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko, na Mpaji thawabu kwa hao wamtafutao kwa bidii.” Kwa hiyo vipi ikiwa kanisa . . .

<sup>135</sup> Hilo ndilo Mungu analotaka. Hilo ndilo Mungu atakalokuwa nalo, kundi la watu wanaoweza kusema, “Yesu Kristo ameahidi nini? Ni kitu gani kilichoahidiwa katika siku hizi za mwisho ambacho hakijadhihirishwa kupitia kwetu?” Amina. Ndipo tunaweza kuketi chini, tumkumbuke Yeye, kumkumbuka Yeye tunapokusanyika pamoja.

<sup>136</sup> Kama kuna kitu chochote tulichopungukiwa, hebu tulifanye. Ikiwa tumepungukiwa na chochote, hebu na turudi kwenye hicho. Hebu tukumbuke kile Yeye alichotaka, sio kile

tunachofikiria tunapaswa kuwa nacho, bali kile Yeye alichosema inatubidi kuwa nacho. Mnaona? Hatuna budi kuwa nacho kwa njia hiyo, jinsi Yeye alivyolisema. Lakini nashangaa kama sisi tunaninii tu...

Tunasema, “Vema, mimi—mimi—mimi ni mfuasi wa *hili*.”

<sup>137</sup> Nashangaa kama unaliwazia kwa uzito, kujua ya kwamba hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Hilo halimaanishi kitu. Herode labda—labda alisema, “Vema, sasa ngoja kidogo tu hapa. Unajua mimi ni nani?” Mnaona? Hakuliwazia kwa uzito. Nasi tunapaswa kuwazia kwa uzito.

<sup>138</sup> Mnajua alichofanya? Wakati Kristo alipowekwa mbele zake, kwa mara ya kwanza, ambapo manabii wote, watu wenye hekima, na kote katika nyakati, ambao walizungumza kuhusu Huyu ajaye. Na hapo Yeye alisimama mbele zake. Mwajua, ninii yake...ninii...Kwenye fursa hii, ambapo Mungu alimweka Kristo mbele ya Herode, yeye aliomba tu burudani.

<sup>139</sup> Nashangaa, ndugu zangu. Hebu tuwazie kwa uzito sasa. Sisi watu wa Kipentekoste, nashangaa kama tunampokea Roho Mtakatifu kwa ajili tu ya burudani? Lakini kuna zaidi ya hicho kinachoambatana Naye. Kuna maisha yanayopaswa kuishiwa. Nashangaa kama hicho ndicho kizuizi cha makanisa yetu leo hii, ndugu zangu. Nashangaa kama hiyo ndiyo sababu tungali huku nyuma nyikani, tukitangatanga, badala ya kuwa huko kwenye Nchi ya ahadi, tukimiliki vitu vyote? Nashangaa ikiwa hakuna kitu fulani hatujawazia kwa uzito vya kutosha kukihusu. Mnaona? Hamna budi kuwazia kwa uzito.

<sup>140</sup> Kama Pilato angalifanya hivyo, angalimwachilia. Kama—kama Herode angalifanya hivyo, angalimwachilia. Bali hakuwazia kwa uzito, fursa yake ya kwanza.

Halafu basi yeye alifanya nini? Aliomba kufanyiwa vitimbi.

<sup>141</sup> Loo, hao, hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Wanataka kuufanya Ukristo vitimbi, kiinimacho kidogo ulicho nacho mkononi mwako. Basi, sikilizeni, enyi Wapentekoste, iweni wanyofu sana katika mambo haya. Mnaponena kwa lugha, na kutoa tafsiri yake, hakikisheni kwamba hiyo ndiyo fasiri. Mnaona? Msifanye kiinimacho. Mnataka kiinimacho cha nini, wakati Mungu ana jambo halisi kwa ajili yenu? Mnaona? Kwa nini mkubali kibadala, huku anga zimejaa yaliyo halisi. Mnaona? Mnaona? Hatuna budi kuwa wanyofu. Haikupasi kujaribu kulipuuza tu na kupita juu yake. Haitupasi kufanya hivyo. Hatupaswi kuomba tupate vitimbi.

<sup>142</sup> Inatupasa kuomba huduma. Amina. “Bwana, kama ninapaswa kuwa mkeka wa mlangoni, nifanye mkeka wa mlangoni ulio bora kuliko yote uliyopata kuwa nayo. Chochote ninachopaswa kuwa, jalia niwe.” Sio, “Nifanye...Kama siwezi kuwa Billy Graham, ama Oral Roberts, mbona, sitakuwa kitu hata kidogo.” Unaona? Mbona, wewe unawaziwa tu sawa na

Billy Graham na Oral Roberts, ikiwa—ikiwa una ninii . . . kama wewe ni mkeka wa mlangoni, kama wewe ni wa Mungu. Mungu anahitaji mkeka wa mlangoni; Yeye—Yeye anataka mkeka mzuri wa mlangoni. Hivyo tu. Mnaona? Haijalishi.

Lakini tunaendelea, tukidhanja ya kwamba tunapaswa kuwa *hiki* ama *kile*. Msifanye hivyo.

<sup>143</sup> Omba tu upate huduma, chochote ilicho. Unaona? Chochote ilicho, acha Mungu achague huduma yako. Unaona? Ndipo basi wakati Yeye anapokupa huduma, kumbuka ya kwamba ni Yesu ndiye aliyekuelekeza hapa. Ulizaliwa kwa ajili ya kusudi hilo. Kuwa m—mtumishi mwema Kwake, popote palipo. Naam.

<sup>144</sup> Yesu alisema, “Kwa nini kuniita Mimi ‘Bwana,’ wala hamyatendi mambo ninayowaambia myatende?” Inatupasa kuyasoma Maandiko. Inatupasa kutafuta kujua ratiba na mpango wa Mungu ni upi. Yeye alisema, “Mnaniita Mimi ‘Bwana.’” Kasema, “Lakini mbona mnaniita Mimi ‘Bwana,’ wakati hamyafanyi mambo ambayo—ambayo ninawaagiza kufanya?” Mnaona? Naam.

<sup>145</sup> *Bwana* ni “umilikaji.” Mwenye nyumba humiliki hiyo a—ardhi. Nao watu, siku hizi, kwa furaha watamkubali Yesu kuwa Mwokozi. Ha—hawataki kwenda kuzimuni. Wata—watamkubali Yeye kama Mwokozi. Bali inapofikia kwenye “Bwana,” loo, la. Ha-ha. Mnaona?

<sup>146</sup> Bwana, ni, wewe kuwa mali Yake. Kama anataka mkeka wa sakafuni, Yeye anakufanya mkeka wa sakafuni. Nawe una furaha tu vivyo hivyo, mkeka wa sakafuni, kadiri vile ungekuwa, nyota ya asubuhi. Mnaona? Mnaona? Mnaona? U—u—unataka . . . Tu—tunataka . . .

<sup>147</sup> Hatutaki kumfanya Yeye “Bwana.” Tunataka Mwokozi, bali hatumtaki “Bwana.” Ndipo akija “Bwana,” na aseme nawe kuhusu mambo fulani ya Neno. “Vema, najua, si—sijui kuhusu Hilo sasa, unaona. Vema, ninii tu . . . Kamwe siwezi kujiwazia nikifanya jambo Hilo,” ninyi kina mama hapa.

Unasema, nitachoka baada ya kitambo kidogo. La. Sitaweza.

<sup>148</sup> Nitakuwa kama yule jamaa alivyosema wakati mmoja, yeye alienda kuhubiri kwenye uamsho mmoja. Alisema alihubiri juu ya toba; usiku wa tatu, toba; usiku wa nne, toba. Alihubiri juma zima juu ya toba.

<sup>149</sup> Ndipo mchungaji wa hilo kanisa na baadhi yao, wakarudi na kumwambia, kasema, “Ndugu, sisi—sisi kweli tunayafurahia mahubiri yako. Lakini hivi huna mengine?”

<sup>150</sup> Kasema, “Loo, naam, bwana.” Kasema, “Ninayo mengine. Lakini acheni wote watubu, ndipo nitahubiri juu ya jambo lingine.” Kwa hivyo, naam, bwana.

<sup>151</sup> Acheni kanisa lianze kwenye ABC zake. Ndipo tutaziendea aljebra basi, jinsi—jinsi ya kuwa manabii, na kuzipata karama, na kadhalika namna hiyo. Lakini hebu kwanza tujifunze hatua hii ya kwanza, kwanza. Ujifunze kutembea kabla hujaweza kukimbia, mwajua. Kwa hiyo, na kama umechoshwa na mtumishi mkaribishaji, utafanya nini? Vema.

<sup>152</sup> Lakini sisi—sisi tunataka kumkumbuka Bwana wetu. Hilo ndilo unalopaswa kukumbuka, kwamba ni Yeye ndiye unayemtumikia. Hampati karama hizi mpate tu kujiburudisha kwazo. Hiyo ni kweli. Hata hivyo, kuna wengi wanaozungumza juu ya karama, ambao nina hakika, kutokana na vile wanavyotenda, hawajui ni kitu gani. Mnaona? Mnaona?

<sup>153</sup> Karama, karama za Mungu, na kadhalika, sio kitu cha kuchezeva tu. Karama za Mungu ni za rehema, na zinachosha. Zinadhoofisha. Hivi Ya-...Katika Uwepo wa Mungu, si kupiga makelele. Ule Uwepo, hizo ni baraka tu za Mungu anazokumwagia. Unaona? Lakini Uwepo wa Mungu ni jambo sumbufu.

<sup>154</sup> Sitaki msahau kuipata hiyo kanda, mkiweza, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Nanyi mkumbuke hilo.

<sup>155</sup> Yakobo, alipolala juu ya ule mto, jiwe, usiku mmoja. Ndipo Bwana akamtokea katika ono, naye akaona Malaika wakishuka na kupanda. Aliposimama, alisema, “Hapa ni mahali panapotisha, si pengine ila ni nyumba ya Mungu.” Mahali pa kutisha!

<sup>156</sup> Wakati nabii Isaya alipokuwa ametabiri kwa miaka mingi, chini ya Uzia. Basi hapo Uzia alipoondolewa kutoka kwake, kwa sababu alijaribu kujitwalia sehemu ya kuhani, ndipo akapigwa kwa ukoma akafa. Naye Isaya labda alikuwa na umri wa miaka arobaini, hamsini. Naye alikuwa ni nabii, loo, tangu utotoni, kwa sababu manabii wanazaliwa. “Karama zao na miito havina majuto.” Naye huyo hapo, na—nabii wa Bwana, huko chini, akiomba, siku moja, na kukiri dhambi zake hapo madhabahuni.

<sup>157</sup> Na mara ghafla, akaja katika Uwepo wa Mungu, na kumwona Mungu ameketi Mbinguni, na vazi Lake. Aliwaona Maserafi huku nyuso Zao takatifu zimefichwa na mabawa, na miguu Yao imefunikwa na mabawa, huku wanaruka kwa mabawa, wakilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi.” Naam.

<sup>158</sup> Ndipo Isaya akakumbuka basi ya kwamba maskini safari yake haikuwa kitu. Alilia nini? Alijua, ka—karama yake, hakuwa ameitumia vizuri. Alikuwa mbali sana. Akasema, “Bwana, mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na ni—ni—ninaishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu.” Ndipo basi Malaika... Mnaona, ni jambo la kutisha. Akasema, “Ole wangu.”

159 Si jambo la baraka, na kupaza sauti, na kupiga mayowe. Hilo ni sawa. Sasa, kumbukeni, silihukumu hilo. Lakini, ninawaambia, hilo silo ninalozungumzia.

160 Ni nguvu na Uwepo wa Mungu, ambao huleta hofu takatifu namna hiyo, hata unapooza katika Uwepo Wake. Daima utakumbuka. Utalikumbuka.

161 Ndipo Isaya akakumbuka, muda wote alioishi. Nawazia, wakati misumeno ilipokuwa ikiukata mwili wake, angali alikumbuka hao Malaika wakiitana, "Mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu!" Bila shaka.

162 Yakobo, katika saa zake za mwisho, angeweza kuwakumbuka wale Malaika wakipanda na kushuka, nalo lilikuwa ni jambo la kutisha sana kwake.

163 Sio kile watu wanachofikiria ndicho. Ni kitu tofauti. Kile tunachohitaji kufanya ni kuingia katika Uwepo Wake, tukimkumbuka, ya kwamba Yeye alituleta hapa sio kwa ajili ya kucheza cheza, bali kwa ajili ya utumishi, akatuleta hapa kumfanyia Yeye kazi.

Alikuwa na jambo la kukumbuka.

164 Vipi kuhusu Yuda Iskariote? Yeye ana jambo la kukumbuka, pia. Yuda analo jambo analokumbuka usiku wa leo. Hakika anakumbuka. Na daima atalikumbuka. Hakika. Kwa nini? Yeye alimwuzwa Bwana Yesu kwa faida ya kibinafsi.

165 Nashangaa, usiku wa leo, kama hakuna wengi wanaofanya jambo lilo hilo leo hii, kuuza haki zako za mzaliwa wa kwanza kwa faida ya kibinafsi, wakati unapaswa kuwa unawaka moto kwa ajili ya Kristo. Wakati unapapaswa kuwa ukimfanyia Yeye jambo fulani, kumfanyia Yeye kazi, ama kitu fulani, unaenda na kujiunga mahali fulani ambapo unaweza kuishi vyovyote utakavyo na ungali unadai kuwa ni Mkristo. Hilo ndilo ulimwengu unalotazamia usiku wa leo. Ulimwengu, nilisema, sio mwaminio.

166 Mwaminio anatazamia kila barabara nyofu anayoweza kupitia, apate kuwa sawa.

167 Lakini asiyeamini anataka mahali fulani anapoweza kwenda na kudumisha maungamo yake ya Mkristo, na halafu aishi tu vyovyote atakavyo. Hilo ndilo taifa hili lililotaka kwa ajili ya rais, na hilo ndilo walilopata. Kweli kabisa. Hilo ndilo—hilo ndilo kanisa linataka, hilo ndilo walilopata. Naam, bwana. Hilo ndilo mnalopata.

168 Lakini mwaminio anataka anyolewe kila kitu. "Anataka kuweka kando kila dhambi, na mzigo umzingao kwa upesi; aweze kupiga mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zake, akimtazamia Mbuni na Mwenye Kutimiza Imani yetu, Yesu Kristo." Naam. Kumkumbuka Yeye, tunapoweka kando kila mzigo. Wanawake wakiziachilia nywele

zao zikue. Wanaume wakiacha kuwa Riki, na kuja kanisani na kufanya yaliyo mema, na mambo haya yote mengine. Na wachungaji wakiwa na mashemasi kwenye halmashauri zao, waliooa mara tatu ama nne; na mambo haya yote, kupatana, kwa sababu wanachangia sana kwenye sahani na yote; hawana budi kujitolea sana kwa dhehebu fulani kwa sababu watakwambia *hili* Ndilo, nayo Biblia inasema kitu fulani tofauti. “Wekeni kando kila mzigo.”

Mkumbukeni Yesu. Akawa asiyepondwa kabisa na watu.

<sup>169</sup> Huyo Rabi kijana alikuwa ni Mmoja wa Watu mashuhuri kuliko wote ulimwenguni, katika siku alipokuwa akiwaponya wagonjwa na kufanya kila kitu vizuri, kuwafanya watu kupona, na kuwafungua macho vipofu, akiwaonyesha watu, na kumdhihirisha Mungu kupitia wao, kwa mawazo ya nia zao wenyewe. Angeweza kuzungumza nao. Yeye alikuwa ni Rabi mashuhuri.

<sup>170</sup> Lakini siku moja aliketi chini akaanza kuwaambia Kweli ya Injili. Hakuwa maarufu tangu wakati huo na kuendelea. La, kamwe hakuwa maarufu. Muda si muda mwajua, na kundi hilo lote likaondoka. Ndipo wale sabini wakasema, “Hili ni jambo gumu. Ni nani anayeweza kulielewa?” Nao wakaondoka.

Ndipo akasimama na kuwauliza hao wanafunzi, “Ninyi nanyi mtaondoka pia?”

<sup>171</sup> Wakasema, “Twende wapi, Bwana? Wewe, pekee. Tumejisalimisha kabisa. Tuko tayari, haijalishi ni nini. Tuko tayari kwenda.” Hebu tumkumbuke namna hiyo.

<sup>172</sup> Kumbukeni, Yeye alikuwa ndiye Mfano wetu. Alifanya kila kitu, akamhukumu kila Mfarisayo, akahukumu kila kitu cha ulimwengu, akapitia ulimwenguni pasipo na doa juu Yake. Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo aliyechunguzwa na Mungu. Yeye alisema, “Huyu ni Mwana Wangu mpendwa. Ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Aliishi maisha ya namna hiyo.

<sup>173</sup> Halafu basi akazichukua dhambi zote za ulimwengu, dhambi zangu na dhambi zako, na kuziweka juu Yake. Ndipo basi hata jasho likatoka kwenye paji Lake takatifu, kama matone ya Damu, yakitapakaa pale. Si kwa sababu kwamba Yeye alikuwa na hatia, bali ni hatia yangu iliyokuwa ikisababisha hilo, na hatia yako.

<sup>174</sup> Na kama Yeye anaweza kufanya hivyo kwa ajili yako na yangu, tungewezaje kusimama chini ya kanuni fulani za imani na upuuzi wa ulimwengu, na mambo ya ulimwengu huu wa kisasa? Inatupasa kumkumbuka Bwana wetu, tukumbuke yale Yeye aliyolipa kwa ajili ya gharama hii ya wokovu. Kamwe tusilionee aibu. “Kuwa tayari kumpa mtu yeyote hesabu kwa ajili ya tumaini lililo ndani yako.” Inatupasa kufanya hivyo, ndugu zangu.

<sup>175</sup> Tunaingia kwenye zile saa za mwisho sasa. Jua linatua. Ustaarabu umekuja kutoka Mashariki. Sasa uko kwenye Pwani ya Magharibi. Hauwezi kwenda mbele zaidi. Kizuizi kiko pale, na dhambi zote za ulimwengu zinalundikana, na kubingirishwa katika mawimbi ya aibu ya Hollywood. Imerudi moja kwa moja kanisani. Basi ni wakati wa namna gani! Inatupasa kukumbuka hilo, ndugu zangu.

<sup>176</sup> Mkumbukeni Bwana wetu. Angefanya nini kama alisimama hapa leo hii? Yeye angelishikilia Neno hilo. Katikati ya kila jaribio, Yeye angekaa na Neno hilo. Alifanya hivyo. Alikuwa ndiye Mfano wenu.

<sup>177</sup> Shetani alipomjia na kusema, “Yageuze mawe haya yawe mkate,” Yeye alisema, “Imeandikwa . . .” Mnaona, daima pamoja na Neno la Baba. Hatuna budi kukumbuka na kufanya jambo lile lile. Yeye alikuwa ndiye Mfano wetu. Naam, bwana.

<sup>178</sup> Makuhani hao wa siku hiyo watakuwa na mengi ya kukumbuka, pia. Wanayakumbuka usiku wa leo katika ulimwengu wa waliopotea.

<sup>179</sup> Mnasema, “Ndugu Branham, ungeweza kuwaita hao makuhani . . .? Makuhani watakatifu, ambao, walikuwa ni watauwa.”

<sup>180</sup> Sasa, ngojeni kidogo. Walijifanya wenyewe watauwa. Walikuwa na utakatifu wa bandia, uchaji wa bandia ambao kweli haukuwa ni wa Mungu. Yesu aliwaambia waziwazi, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mtazifanya.” Basi akawaambia kile walichokuwa. Nao wanayo mengi ya kukumbuka, pia. Kwa sababu, walipoona hilo dhihirisho halisi la Masihi, akithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, walilikataa makusudi na kusema Hilo lilikuwa ni pepo mchafu akifanya hilo. Kasema, “Ilikuwa ni Beelizebuli.”

<sup>181</sup> Naye Yesu akatamka kwamba huko kulikuwa ni kukufuru. “Yeyote atakayesema neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa kamwe.” Wanayo mengi ya kukumbuka. Hebu tusipachukue mahali pao, ndugu. Hebu hatima yetu isiwe kama yao.

<sup>182</sup> Lakini ikinibidi kuwa, acheni niwe kama Nathanaeli, akisema, “Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Hebu nisimame kama mmoja wa hao. Hebu nisimame.

<sup>183</sup> Hebu nyinyi wanawake msimame kama yule mwanamke kisimani, anavyosimama usiku wa leo. Anayo mengi ya kukumbuka, kama tulivyozungumzia. Alipata chemchemi.

<sup>184</sup> Na sasa, hao makuhani, watakuwa na ninii . . . Ni kwa nini wakafanya hivyo? Kwa sababu ya wivu dhahiri kabisa. Ni hivyo tu. Walikuwa na bidii ya kanuni yao ya imani. Walikuwa nayo. Walikuwa na bidii ya mapokeo yao. Wazee wao walikuwa

wameweka mapokeo yaliyokuwa ni kinyume cha Neno, nao walikuwa na bidii ya mapokeo hayo.

<sup>185</sup> Ndugu, hebu mimi na wewe isitulazimu kuwajibika kwa hilo, bidii ya mapokeo yoyote. Hebu na tumkumbuke Yesu, kile Yeye alichokuwa. Tudumu na yale Yeye aliyosema. Kwa wivu halisi waziwazi, walifanya mambo haya. Loo, ni jambo la jinsi gani! Naam, bwana. Wao...

<sup>186</sup> Yule tajiri ana mengi ya kukumbuka, pia. Alipewa nafasi ya kumpokea Yesu Kristo, bali alipenda sifa za wanadamu kuliko sifa za Mungu. Basi, kumbukeni, Biblia inasema dhahiri ya kwamba yeye alikumbuka hilo akiisha kufa na yuko kuzimuni, nao ule ujumbe ukamrudia, "Kumbuka, katika maisha yako, ulikuwa na nafasi."

<sup>187</sup> Nanyi Phoenix, mnayo nafasi. Ulimwengu unayo nafasi. Usiache ivukie njia yako nawe ukose kuiona, kama vile Herode na—na wengi wao walivyofanya.

<sup>188</sup> Sasa, wanaonyesha ya kwamba kwa kweli hao makuhani walijua kwamba Yeye alikuwa ni Nani, maana Nikodemo alilielezea wakati alipokuja. Yeye alikuwa ni mmoja wa viongozi wa Mafarisayo. Alisema, "Rabi, tunajua ya kwamba Wewe ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo hayo isipokuwa Mungu awe pamoja naye." Mnaona, walijua jambo hilo. Lakini, mnaona, hawana budi kukumbuka hilo. Walijua vema zaidi, bali hawakulifanya.

<sup>189</sup> Unaacha kanuni yako ya imani ikufinyilie chini, kutoka kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa sababu wanakwambia hakuna kitu kama hicho.

<sup>190</sup> Hapa miezi michache iliyopita, nilikuwa huko nje hospitalini kumwomba mwanamke fulani, katika mji wetu huko Indiana. Basi palikuwapo na maskini mwanamke mmoja amelala pale, alitaka kujipatanisha na Mungu. Alikuwa...Alikuwa amerudi nyuma. Wakati mmoja alikuja kwenye kanisa langu. Akarudi nyuma akatoka. Ndipo, hakika, pepo saba wakaingia, wabaya kuliko walivyowahi kuwa. Naye huyo hapo amelala, hospitalini, yuafa.

Akasema, "Ndugu Branham, sitaki kufa jinsi hii."

<sup>191</sup> Nami nikasema, "Vema, dada. Haikupasi, kama ungali na shauku moyoni mwako ya kumtumikia Mungu. Kamwe hajawahi kukuacha. Wewe ulimwacha, bali Yeye kamwe hakukuacha. Sasa unaweza, kama ukiweza."

Akasema, "Na—nataka kurudi, Ndugu Branham."

Nikasema, "Vema, tutaomba."

<sup>192</sup> Palikuwapo na mama mwingine aliyelala hapo, ameinamisha midomo yake, akaniangalia kwa ninii...kana kwamba angenivamia mimi, naye pamoja na mwanawe. Alikuwa amelala kitandani; akienda kufanyiwa upasuaji,

siku moja kabla. Basi nikasema... Nami nilimwona akienda, akimwangukia mwanawe, akiniangalia mimi.

<sup>193</sup> Basi—basi nikasema, “Utajali kama tukiomba dua kidogo?”

Akasema, “Vuta pazia hilo.”

Nikasema, “Vema, mimi... Hivi wewe ni mwaminio?”

Akasema, “Nilisema, ‘Vuta pazia hilo.’”

Nikasema, “Nilikuuliza tu.”

Akasema, “Nataka uelewe, sisi ni Methodisti.”

Nikasema, “Vema, hilo bila shaka linalielezea basi, unaona.”  
Mnaona?

<sup>194</sup> Ilikuwa ni kitu gani? Hakutaka kumwona mtu mwingine, huyo maskini mwanamke aliyerudi nyuma, akimrudia Mungu. Sasa, angalikuwa ni Mmethodisti, ingalikuwa ni tofauti, mnaona. Hakumkumbuka Yesu pale, mnaona. Alikumbuka tu kanuni yake ya imani.

<sup>195</sup> Kumbukeni tu. Vema. Loo, litakuwa ni jambo la kuogofya jinsi gani katika Siku hiyo ya Hukumu.

<sup>196</sup> Majuma machache yaliyopita nilikuwa nimepanda lifti huko Louisville. Nilikuwa nikienda kufanyiwa uchunguzi, uchunguzi wa mwili, kwa daktari rafiki yangu, kupata pa—pa—pasi, kusudi nikitaka kwenda nchi za ng’ambo pamoja na Ndugu Rowe na hao wengine mara moja. Na kwa hiyo nikawazia ningefanyiwa uchunguzi wangu wa mwili wakati nikiwa na nafasi, ndipo nikapanda juu.

<sup>197</sup> Pa—palikuwapo na wanaume fulani pamoja nasi, wakipanda orofani. Tukaenda juu sana, yapata orofa nane, huko Louisville, na kwenye jengo, na, kwa hiyo, lile jengo la Heyburn. Basi nilipokuwa juu sana kadiri tulivyoweza kwenda, kusimamisha, hawa... Mmoja wa jamaa hawa alikuwa akinywa kidogo, nafikiri. Akaangalia kote, kasema, “Vema, enyi wavulana, nadhani hii ni juu kiasi kile tutakachowahi kufika.” Kasema, “Afadhali tutoke.” Kamwe sikusema chochote. Yeye hakujua nilikuwa ni mhubiri. Kwa hiyo, nilingojea tu kutoka.

<sup>198</sup> Nikasema, “Hebu kidogo. Tamshi hilo ulilotoa.” Nikasema, “Ikiwa tunategemea ustadi wetu wenyewe, hii ndiyo juu kiasi kile tutakachowahi kupanda, lakini,” nikasema, “iwapo tutamategemea Yesu! Tumkumbuke Yeye.” Amina.

<sup>199</sup> Tunaweza kwenda juu zaidi, tunapopita, kama vile waimbaji wa Ndugu Outlaw walivyosema hivi majuzi usiku, Jupita, Zuhura, Neptuni, Marsi, Kilimia Nyeupe, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea. Hakuna tofauti. Kupita kila mfumo wa jua, kuingia mbingu za Mbingu! Ninafurahia jambo hilo.

<sup>200</sup> Kumbukeni tu ya kwamba Yeye alipaa juu na juu ya vitu kama hivyo. Naam. Kama tukitegemea ustahilifu wetu,

hakika tumepotea. Lakini kama tukitumainia ustahilifu Wake, tumeokoka.

<sup>201</sup> Loo, tunaweza kumkumbuka Yesu katika neema Yake, kwamba Yeye alituinua juu na akaahidi hilo, ya kwamba, hata sasa, sasa hivi, haitubidi kuwa wanaoelekea duniani. Mnaona? Sisi hatuelekei duniani sasa. Tunaelekea Mbinguni. “Tayari tumekufa. Uhai wetu umefichwa ndani Yake, kwa njia ya Kristo.” Nasi tumefufuka pamoja na Yeye; sio, sisi hatuninii—hatujafa pamoja na Yeye. “Tumefufuliwa pamoja na Yeye, nasi tumeketi mahali pa Mbinguni.”

<sup>202</sup> Kumkumbuka Yeye, tumeketi mahali pa Mbinguni! “Lini, Ndugu Branham?” Sasa hivi. Naam. Hatutafufuliwa pamoja na Yeye. Tayari tumefufuka pamoja na Yeye. Haya ni Malimbuko ya kufufuka kwetu: tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nasi tu hai milele; tumeketi mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tayari tumefufuliwa pamoja na Yeye kutoka kwa wafu. Naam. Ni jambo tukufu jinsi gani kuketi mahali pa Mbinguni pamoja na—pamoja na Yesu Kristo, Mwana wa Mungu! Naam, bwana. Tunaweza kumkumbuka sasa, na ahadi Zake zote alizotufanyia sisi, wakati tunapoketi papa hapa sasa.

<sup>203</sup> Nilikuwa nikiangalia ile saa ya ukutani pale nyuma, nami nikawazia, “Jamani, ninafanya vizuri sana. Niko karibu kumaliza hapa sasa, saa moja.” Nilikuwa na yapata kurasa tatu zaidi za muhtasari, nami nikazisukumia nyuma chini *pale*. Nilipoangalia saa yangu ya mkono, ndipo nikaona haikuwa imefika saa moja. Kwa hiyo nikawazia, “Ninafanya vizuri sana.” Nimekuwa wapi? Nimekuwa nimepotea muda huu wote? Nilijua ni—nilijisikia vizuri sana, lakini sikujua nilijisikia vizuri hivyo. Na—nami ningeninii. . . Niliendelea kuiangalia saa ya ukutani, nami nikawazia kuna kasoro, mahali fulani.

<sup>204</sup> Vema, hivyo ndivyo itakavyofanyika, moja ya siku hizi, enyi marafiki. Wakati utasimama. Nasi tutaruka hewani tuingie katika Umilele, ambamo hamna wakati tena. Hilo si litakuwa ni ajabu?

<sup>205</sup> Lakini wakati tukiketi hapa sasa, ambapo wakati hauna maana kwetu, tayari tumeinuliwa tukaingia mahali pa Mbinguni. Tunaweza kukumbuka nini? Tunaweza kukumbuka kila ahadi aliyotufanyia. “Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu likae ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo.” Hiyo ni kweli?

<sup>206</sup> Ninaweza kukumbuka Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kuamini,” sio kujifanya anaamini, sasa, bali, “kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna,” huo ni wakati uliopo, “Uzima usio na mwisho, wala hataingia katika lawama ya Hukumu, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Nasi tunaishi sasa hivi katika Kristo Yesu, tumeketi

katika mahali pa Mbinguni. Hilo ndilo aliloahidi. Tunaweza kukumbuka.

<sup>207</sup> Tunaweza kukumbuka jinsi alivyosema, alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi miongoni mwa watu. Waaminio waliona jambo hilo. Nasi tunakumbuka, katika Yohana Mtakatifu 14:12, ya kwamba Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.” Tunaweza kukumbuka Yeye aliahidi hilo.

<sup>208</sup> Tunaweza kukumbuka Yeye aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba Roho Mtakatifu angejidhihirisha katika mwili wa binadamu, kama vile hasa Yeye alivyofanya katika Sodoma kabla haujateketezwa. Tunakumbuka Yesu alifanya ahadi hiyo. Ninaikumbuka. Yeye alisema hivyo. Yesu alisema hivyo. Ninaliamini vile vile tu, kama ningalikuwa nimeketi pale na Yeye akaniambia kulihusu, maana lipo papa *Hapa*, na hivyo ndivyo ninavyoliamini Neno hilo. Ninakumbuka Yeye alisema hivyo. Hayo ndiyo yote.

“Kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya.”

<sup>209</sup> Ninakumbuka, nilikuwa nikisoma katika Maandiko, hivi majuzi usiku, ambapo Yesu alisema, wakati, “Ninayo mambo mengi ya kuwafunulia, kuwaambieni. Lakini, ninyi, siwezi kufanya hivyo sasa. Lakini ajapo Roho Mtakatifu, mnaona, Yeye atawakumbusha mambo haya, na kisha Yeye atawaonyesheni mambo yajayo.”

<sup>210</sup> Nakumbuka ya kwamba Roho Mtakatifu alinena na kusema, “Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga wowote ukatao kuwili, linachoma hata kugawanya viungo na mafuta yaliyomo, na ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo.”

<sup>211</sup> Ninakumbuka ya kwamba Yesu alipitia kwenye umati siku moja, na maskini mwanamke mmoja akaligusa vazi Lake. Kisha akaenda huko nje na kuketi chini, na huko nje, akasimama, ama popote alipokuwa. Ndipo Yesu akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

<sup>212</sup> Wakati, Petro alifikiri alikuwa amerukwa na akili Zake. Akasema, vema, akamkemea na kusema, “Vema, kila mtu anakugusa.”

<sup>213</sup> Yeye akasema, “Lakini naona. Nimekuwa mnyonge. Nguvu zimetoka.” Akaangalia kila mahali. Akampata maskini mwanamke huyo, akamwambia, “Kutokwa kwake damu. Imani yake ilikuwa imemwoko.”

<sup>214</sup> Ninakumbuka ya kwamba Biblia inafundisha, katika Waebrania, ya kwamba Yeye sasa ni Kuhani Mkuu, loo, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli.

<sup>215</sup> Ninakumbuka Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8. Ninakumbuka Yesu. Yeye alifanya. . . Katika Waebrania 13:8, Yeye alisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Loo, jinsi tunavyoweza kumkumbuka Yeye! Naam, bwana. Loo, jinsi sisi. . .

<sup>216</sup> “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona,” Kanisa, mwaminio, “kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Hiyo ni kweli. “Sitawaacha kamwe.” Loo, sio tu kitu kinachotendeka leo na kutoweka kesho. Ni cha Milele. “Sitawaacha kamwe. Sitawapungukia.” Loo, jamani! Hilo lingetufanya tupige mayowe, tupaze sauti, tulie.

<sup>217</sup> Tunataka kuzingatia hili kwa makini. Mkumbukeni Yesu, sio tu kwa njia ya kiholela. Yeye aliahidi jambo hili. Na iwapo hilo halifai kitu, basi Biblia haifai kitu. Basi tunaketi hapa kwa sababu gani? Hata tunaishi kwa sababu gani? Unajaribu kwa sababu gani? Jitihada zako ni za nini? Kwa nini unalitolea jasho? Kama ni kweli yoyote, hata kidogo, ama kila sehemu yake ni kweli au hakuna yoyote yake iliyo kweli. Kumbukeni, haikuwa ni mimi au wewe, ama wachungaji wenu, waliotoa ahadi. Ilikuwa ni Yesu ndiye aliyetoa ahadi hizi. Ninakumbuka Yeye alisema hivyo.

<sup>218</sup> Ninakumbuka Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Umbali gani? “Ulimwenguni kote.” Naam. Theluthi mbili zake hazijui kitu kumhusu Kristo bado. “Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ninakumbuka Yeye alisema hivyo. Kama ninaweza kukumbuka hilo, ninawezaje kukubali kitu, basi, kinachosema ya kwamba siku hiyo imepita? Ninakumbuka Yeye alisema, “Ulimwenguni kote, kila kiumbe. Nazo ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

<sup>219</sup> Ninawezaje kujiweka pamoja na kundi la watu wanaolikana Neno hilo, wakati Mungu alikuwa akiliangalia Neno Lake, apate kulithibitisha? Ninawezaje kujishikamanisha na wasioamini?

<sup>220</sup> Ee Mungu, jalia nimekumbuke Yesu. Jalia nikumbuke msimamo aliochukua. Jalia nikumbuke ya kwamba Yeye ni Mwokozi wangu. Jalia nikumbuke ya kwamba mimi nimekufa. Siko tena. Nimekuwa nimekufa miaka thelathini na mitatu. Huyu ni Kristo aishiye ndani Yangu.

<sup>221</sup> Na kama nikiangalia na kumwona akifanya mambo yasiyo ya kawaida, yasiyo mema, basi ninajua kwamba kamwe sikufa; William Branham angali hai; wewe ungali hai. Mradi tu huzitii amri Zake, basi wewe ungali hai. Lakini wakati unapozishika amri Zake, “Mkinipenda, zishikeni amri Zangu.”

<sup>222</sup> Ni ajabu jinsi gani, kuwazia kwamba Yeye aliahidi hili! “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Ulimwengu hautaniona, bali hata hivyo ninyi mtaniona.” Loo! “Walipo wawili au watatu wamekusanyika pamoja, nitakuwa miongoni mwao.” Ninakumbuka hilo. Mnakumbuka hilo, ndugu zangu? [Ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.]

223 “Na kazi nizifanyazo Mimi, hao nao watazifanya.” Yeye alifanya kazi za aina gani? Haya basi. Mnaona?

224 “Loo, vema, hakika, sasa, Ndugu Branham, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine. Si—si hivyo.”

225 Ninakumbuka hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Sikumbuki yale wewe uliyosema. Hayo yote yamepita, mnaona, bali ninakumbuka aliyosema. Mnaona? “Yeye atakayenifuata Mimi atajikana mwenyewe,” ayakane mawazo yake mwenyewe, akane mawazo yake mwenyewe. Ungeweza kumkana baba yako, mama yako, mke wako, watoto wako; lakini kuna jambo fulani lililo halisi sana hata huwezi kulikana Hilo. Linakuhifadhi. Na Yeye yupo hapa.

226 Sasa hebu tukumbuke tu kila ahadi aliyofanya, tunapoviinamisha vichwa vyetu.

227 Baba yetu wa Mbinguni, kulikuwako na haja nyingi dakika chache tu zilizopita. Mikono iliyoinulia ilitokeza kote jengoni. Lakini, Baba, Wewe ni Mungu aliye hai. Nami nakuomba, Bwana Yesu, kuwabariki watu hawa. Jalia Roho Wako Mtakatifu aishi juu yao, awape Uzima wa Milele, awape wanachohitaji.

228 Jalia tukumbuke, Wewe ulifanya ahadi. Wewe ndiwe unayewajibika kwa ajili ya ahadi hii. Jalia tukumbuke, haijalishi mtu yeyote mwingine anasema nini, Wewe Ndiwe. Wewe Ndiwe tunayemtazamia, kuitimiza ahadi Yako. Wewe Ndiwe uliyesema, ya kwamba, “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa hata hivyo ataishi. Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.” Ninakumbuka Wewe ulisema hivyo, Bwana.

229 Halafu Wewe ulisema, wale waliokuamini Wewe... Sasa, Wewe ulisema, kama tukiamini, tungelikuwa na Uzima wa Milele. Nawe ulisema, hao waliokuamini Wewe, kazi ulizofanya Wewe wangezifanya pia.

230 Sasa, Baba, tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu, nasi tunajua ya kwamba hakuna mwingine ila Wewe. Nasi tunakuamini Wewe, na tunakutumainia Wewe sasa, katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa.

231 Ni wangapi walio katika jengo hili wanaojua ya kwamba humkumbuki Bwana wako katika njia unayopaswa kumkumbuka? Na mwishoni mwa maskini Ujumbe huu, uliokatikakatika, mko tayari kuinua mikono yenu na kusema, “Mungu, jifanye halisi sana kwangu hata nitakukumbuka juu ya ninii yangu... Amri Zako zitakuwa kwenye nguzo ya kitanda changu? ‘Nimemweka Bwana mbele zangu daima,’ kama Daudi alivyosema. Bwana, nipe nafsi Yako zaidi, nipate kukukumbuka.” Inua mkono wako, useme, “Niombee, ndugu.” Hilo ni karibu kila mahali kwa kauli moja. “Bwana Yesu, unirehemu.”

<sup>232</sup> Sasa, kuna wale hapa usiku wa leo ambao kamwe hawajawahi kumkiri Yeye kama Bwana wenu? Na sasa mnaweza kusimama mbele Zake... Nasi tumewaambia, dakika chache tu zilizopita, ya kwamba Yeye aliahidi, ya kwamba, “Walipo wawili au watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao.” Sasa, Yeye aliahidi hilo. Basi, hana budi kuwa hapa. Nawe hujawahi kumkubali Yeye kama Bwana wako?

<sup>233</sup> Utafanya jambo hilo la kipumbavu alilofanya Herode? Utachukua msimamo huo ambao Pilato alichukua, kumsukumia mbali kwa mtu mwingine? “Mama yangu, alikuwa Mkristo. Baba yangu yuna dini ya kutosha kwa ajili yetu sote.” Ungefanya hivyo? “Mke wangu ni mwanamke wa kidini.”

<sup>234</sup> Na wewe vipi? Waweza kuinua mikono yako na useme, “Mungu, unikumbuke. Mimi ni mwenye dhambi, nami ninataka kujipatanisha na Wewe. Nitainua mkono wangu”? Ni mikono mingapi hapa ndani iliyo namna hiyo? Kuna ninii... Mnataka kusema hakuna mwenye dhambi humu jengoni? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama, hapa. Haya basi. Nilifikiri kulikuwako na kitu kilichokuwa kikivuta kwa makosa hapa. Mimi... .

<sup>235</sup> Mnaelewa, ya kwamba, Yesu alisema Yeye alikuwa hapa. Na Yeye anayajua mawazo yako, unaona, moyoni mwako. Asanteni kwa uaminifu wenu. Kwa kweli, wapo wengi ambao wanapaswa kuinua mkono wao.

<sup>236</sup> Lakini waweza kuinua mkono wako basi? Useme, “Ni... . Ndugu Branham, ni—ninatekeleza tu sehemu ya unafiki. Mimi huenda kanisani. Lakini inapofikia hasa kuzaliwa mara ya pili, nilijiunga tu na kanisa. Kweli simjui Kristo. Ningali ninaupenda ulimwengu kadiri tu nilivyowahi kuupenda. Ni—ninaninii tu... . Loo, ninafurahia kwenda, kuusikiliza ujumbe ama kitu fulani. Lakini inapofikia hasa kuchukua wakati na kupenda kutoka nje, na kuzitumia saa hizo katika maombi pamoja na Yeye, na kushiriki na Yeye, nikimkumbuka, si—sifanyi hivyo. Hata sina shauku ya kufanya hivyo. Ninajua basi, Ndugu Branham, siwezi kuwa sawa na kuwa na hisi ya namna hiyo. Kwa hiyo, ninamwinulia Mungu mkono wangu, ‘Unirehemu.’” Inua mkono wako. Kuwa mnyofu nao. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Bwana akubariki. Amina.

<sup>237</sup> Ninangojea tu, nione kama Roho Mtakatifu atafunua jambo lingine. Mungu akubariki bwana. Mungu akubariki. Hakika. Ninamtaka tu Yeye auchunguze moyo wako. Hilo ndilo lililomleta hapa. Vema. Mungu akubariki, msichana. Hilo ni jambo zuri sana.

Wakati tu ukiliwazia, lichukue kwa uzito sasa.

<sup>238</sup> “Loo, Ndugu Branham, si—sina budi kwenda nyumbani haraka.” Sikiza. Utaharakisha utoke kwenye maisha haya, siku

moja, pia. Unaona? Liwazie sasa. Haya ndiyo majira. Huu ndio wakati.

<sup>239</sup> Sema, “Vema, nakwambia. Mchungaji wetu, yeye ni—yeye ni mtu mwenye akili sana, amesoma sana. Afadhali nisikie kutoka...”

<sup>240</sup> Haileti tofauti yoyote ni nani anayeuleta Ujumbe. Sio—sio mjumbe. Ni Ujumbe ndio unaosikia. Unaona? Haijalishi ni mtu wa namna gani angeingia pale mlangoni na—na kukupa ujumbe kwamba—kwamba wewe—ulirithi dola milioni moja, ungezikubali hi—hizo pesa. Ukubali msamaha wako.

<sup>241</sup> Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, na macho yenu yamefumbwa, nitawauliza jambo fulani kwa unyofu kabisa. Nami ninawatakeni mniambie ukweli.

<sup>242</sup> Enyi wanawake, ninyi mlio na nywele fupi, ni wangapi wanaojisikia kweli kwamba inawapasa kuwa na nywele ndefu? Inua mkono wako na useme... Mungu awabariki. Hilo ni jema. Ninajua mlifanya hivyo. Mimi—mimi... Kuna matumaini kwa ajili yenu. Lakini wakati mmechomwa moto kabisa, hata hamwezi kulifanya, hata hamjisikii kuhukumiwa, mnaona, basi kuna jambo fulani lililotukia kwenu. Kwa sababu, Neno lilisema inawapasa.

<sup>243</sup> Ni wangapi, ninyi wanawake, wanaovaa kaptura na nguo hizo, ama kuvuta sigara; na—nanyi wanaume, pia, mnaojua ya kwamba mnafanya makosa? Na unasema, “Sitaki kufanya hivyo, Ndugu Branham. Kweli ninampenda Mungu, lakini ki—kitu hicho kinanishikilia tu. Nami ninajua ni kitu kiovu. Nitainua mkono wangu. Katika—katika kuinua mkono wangu, ninamwomba Mungu akiondoe kwangu.” Inua mkono wako. Kuwa mwaminifu. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli. Naam. Hiyo ni kweli.

<sup>244</sup> Huo ni uaminifu. Huo ni ukweli. Mungu atatupa mkutano wa uponyaji katika dakika moja, juu ya uaminifu huo. Tunaweza kuamini hilo. Mwaminini Mungu.

<sup>245</sup> Baba wa Mbinguni, umeiona mikono hiyo. Unazijua hali za hao watu. Unajua yale yote yaliyo mioyoni mwao, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utaleta msamaha wa dhambi kwa kila mmoja wao. Basi, sasa, wape shauku ya moyo wao. Ondoa huzuni zao. Fanya hivyo, Bwana, ambalo wana haja ya kujua. Ninaomba ya kwamba utawajalia, kupitia Jina la Mwana Wako mpendwa, Bwana wetu Yesu. Tunaomba hayo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Ninawakabidhi Kwako, Baba Mungu, ili Wewe ufanye kazi Yako ndani yao, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>246</sup> Sasa, unapoinua kichwa chako. Ni wangapi wanaojisikia tofauti sana kulihusu, inua tu mkono wako, useme, “Ninajisikia tofauti kabisa.” Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba

Yeye aliahidi ya kwamba Yeye—Yeye ni “Bwana ayaponyaye magonjwa yetu yote”? Mnaamini hilo? Ungeamini?

247 Ni wangapi wenu wanaamini ya kwamba Yeye aliahidi hili, kwamba, “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona Mimi”? Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini inawezekana basi, kama Waebrania 13:8 hapa ilivyosema, “Yesu Kristo, yeye yule jana na hata milele,” mnaamini inawezekana ya kwamba tungeweza kumwona Mungu? [“Amina.”] Tungemwonaje? Katika dhihirisho la Roho Wake, Utu Wake ulio hai. Mngeamini hilo? [“Amina.”]

248 Nitawaomba ndugu zangu wasiombe juu ya jambo hili, huko nyuma. Ila tu, mniombee mimi. Acheni kusanyiko, wakati huu. Tunakuja kwenye mkutano katika siku chache, nasi huenda tutalishika hilo.

249 Ninalitaka kusanyiko hili katika udhibiti mmoja. Ninataka kuchukua roho hizi chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wake, ili Roho Wake aweze kutenda kazi na kuthibitisha ya kwamba Yeye angali hai.

250 Ninalichukua Neno Lake hapa. Lilisema kwamba, Yohana Mtakatifu, Yohana Mtakatifu mlango wa 14 na kifungu cha 12, ilisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

251 Halafu, kila mmoja wenu ninyi watu huko nje, mlio wagonjwa au wahitaji, ama mna haja ya jambo fulani, ombeni. Gusa tu, kumbukeni, upindo wa vazi Lake. “Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

252 Je, Biblia inasema hivyo, ndugu? [Ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.]

253 Halafu Yeye angetenda namna gani, kama Yeye alikuwa ndiye Kuhani Mkuu? Jinsi vile alivyotenda wakati Yeye alipokuwa hapa, maana Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Angefanyaje jambo hilo? Wakati mwili Wake ndio dhabihu kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, angeweza kufanya hivyo? Yeye alimrejesha Roho Wake, Roho Mtakatifu. “Naye atachukua mambo yaliyo Yangu, na kuwaonyesha ninyi.” Sasa, ukitaka kuona kama Mungu . . .

254 Sababu ya mimi kuweka msingi hili juu ya jambo hili, nikijua hivi, najua ya kwamba Ujumbe ninaowahubiria watu ni Kweli. Ni—ni—ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Ingawa, Huo unakatakata *hapa*, kidogo namna *hiyo*; sio kuwa katili, sio kuwa tofauti, bali kuwa mwaminifu. Na, kwa hiyo, ninajua Yeye alisema hilo. Kama angechukua mambo yaliyokuwa ya Mungu . . . Na hili linapaswa kukufanya ujue hilo. Kama akichukua mambo yaliyo ya Kristo, na kuwaonyesha nyinyi, na

kuwaonyesha mambo yajayo, na kufanya kazi zile zile alizofanya Yeye, huyo ni Roho Mtakatifu. Haina budi kuwa hivyo.

255 Ombeni sasa, na mliguse vazi Lake. Nitajitolea mwenyewe Kwake, nione yale Yeye atakayowaambia. Ombeni tu.

256 Kuna wengine hapa ambao kamwe hawajawahi kuwa mkutanoni hapo awali? Waweza kuinua mkono wako? Naam, wapo wengi.

257 Kumbukeni, Yesu Kristo kamwe hata wakati mmoja hakudai kuwaponya watu. Alisema, “Si Mimi ninayezitenda hizi kazi. Ni Baba Yangu,” na katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 5 na kifungu cha 19.

258 Wakati Yeye alipopitia kwenye birika la Bethesda, na kulikuwako na umati mkubwa waliokaa pale, ya idadi ya watu, labda maelfu wamelala pale, viwete, vipofu, vilema, waliopooza, Yeye alimwendea mtu ambaye labda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume, ama huenda alikuwa na kifua kikuu. Ulikuwa umedumaa. Alikuwa amekuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane. Basi Yeye akamwambia, “Jitwike kitanda chako uende nyumbani.”

259 Mtu huyo angeweza kutembea. Alisema, “Wakati ninaposhuka mimi, mtu mwingine. . .” Na palikuwapo na watu hapo waliokuwa hali mbaya zaidi kuliko alivyokuwa yeye.

260 Lakini Yesu alijua ya kwamba alikuwa pale, na alijua alikuwa katika hali hiyo. Wakati alipohojiwa, Yeye alisema, “Amin, nawaambieni, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe. Ila lile ambalo Yeye amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile.”

261 Huo ndio msimamo Wake ule ule leo hii. Hakuna nabii, hakuna yeyote aliyewahi kuwa na uwezo kufanya lolote nje ya mamlaka ya mapenzi ya Mungu, hiyo ni kweli, atakayo Mungu.

262 Sijui. Ninataka, kama . . . Hiyo ndiyo sababu. Ninajua baadhi la wahudumu hawa wanaoketi hapa. Hapana wengi sana *pale* nje ninaowafahamu. Kama nikimwona Yeye juu ya mtu fulani, ningejaribu, kama akipenda, nitawaambia watu kwamba niliwajua.

263 Ninyi ombeni, mwone kama Yeye angali ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa. Hilo lingemweka Yeye papa hapa mbele zetu, nanyi mngeona kwamba Yeye yupo hapa. Hiyo ni kweli? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bila shaka ingemfanya kuwa hapa. Iweni tu na imani.

264 Huyu hapa maskini mama mmoja ameketi papa hapa huku ameinua kichwa chake hewani, akiomba kwa nguvu awezavyo. Amevaa koti la kijani kibichi, ameketi papo hapo. Anaomba ugonjwa ulio kichwani mwake. Kwamba yeye . . . Unaomsumbua. Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako kama

hiyo ni kweli. Kama mimi ni mgeni kwako, punga mkono wako huku na huko. Umekuacha sasa.

<sup>265</sup> Aisee, utanipa fadhila wakati ukiwa hapo? Nuru hiyo ilisonga moja kwa moja juu ya mama huyo anayeketi karibu nawe hapo. Anaomba pia. Ninataka kukuuliza jambo fulani. Ulisema, “Unikumbuke, Bwana.” Vema, Yeye amekukumbuka. Unaugua uvimbe wa pua. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, na upunge mkono wako. Vema. Haya basi. Mnaona?

<sup>266</sup> Mnaamini? Sasa, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena.” Waulizeni hao wanawake. Mnawaona. Waulizeni kama ninawajua.

<sup>267</sup> Hapa, huyu hapa kijana mwanamume ameketi hapa, akimwombea baba yake. Kamwe sikukufahamu. Sijui wewe u nani. La. Sijui lolote kukuhusu. Lakini unamwombea baba yako. Hayupo hapa. Yuko ng’ambo ya maji mengi mno mahali fulani. Anaugua ugonjwa wa tumbo. Yuko Puerto Rico. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Amini.

Mnaona ninalomaanisha?

<sup>268</sup> Huyu hapa mama mmoja ameketi hapa, anaonekana kuvutiwa, kofia nyekundu. Bibi Aldridge, Aldridge. A-ha. Naam. Anaugua ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema.

<sup>269</sup> Utanipa fadhila? Yupo mama anayeketi karibu na hapo, jina lake, Bibi Cook. Bibi Cook ana shida na miguu yake. Hiyo ni kweli. Bibi Cook, inua mkono wako. Kama mimi ni mgeni kabisa, inua mkono wako. Vema. Mwamini Mungu.

<sup>270</sup> Weka mkono wako juu ya mwanamke aliye karibu naye. Yeye ni Bi Russell. Anaugua ugonjwa wa pafu. Inua mkono wako, Bi Russell, na uamini kwa moyo wako wote, iwapo hunifahamu mimi.

<sup>271</sup> Vipi kuhusu huyo anayefuata? Naam. Kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni imani.

<sup>272</sup> Mama huyo aliye karibu naye anaugua ugonjwa wa tumbo, pia, na jina lake ni Bibi Dillman. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza.

<sup>273</sup> Bibi Harmon, anayeketi karibu naye, ndio kwanza atoke hospitalini. Amekuwa na u—upasuaaji kwa ajili ya—ya ugonjwa wa rektamu. Unaamini, Bibi Harmon? Iwapo unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda nyumbani, upate afya.

<sup>274</sup> Ni wangapi wanaoamini sasa?

<sup>275</sup> “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena.” Halafu basi ninajaribu kusema nini? Kumbukeni, Yesu aliahidi. Yesu alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi

nanyi mtazifanya.” Tukikumbuka Yesu aliyaahidi mambo haya, Yesu anayatimiza.

<sup>276</sup> Sasa, pia, kumbukeni ya kwamba Yesu aliahidi, ya kwamba, “Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele.” Wewe uliyeinua mkono wako, muda mfupi uliopita, baada ya ibada hii ya uponyaji waweza kupanda hapa sasa na kusimama hapa kwa ajili ya maombi? Yeye aliahidi kutoa Uzima wa Milele kama vile alivyoahidi uponyaji.

<sup>277</sup> Sasa, hivi mlifua aliahidi hili pia? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa watapata afya.” Unaamini hilo? Sasa wekeni mikono yenu mmoja juu ya mwingine basi. Mnaona, Yeye yupo hapa. Siwezi kuwaponya. Tayari amewaponya. Sasa weka mikono yako juu ya mtu fulani, na umwombe mtu fulani, papo hapo karibu nawe hapo. Amina.

<sup>278</sup> Sasa inamisheni vichwa vyenu na kuomba tu kama vile mfanyavyo kanisani mwenu. Omba, “Bwana Mungu, mponye mtu huyu. Mtu huyu ananiombea.” Na umwombe tu Mungu kumponya na kumpa afya. Amini kwa moyo wako wote. “Bwana, ninamwamini Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Neno Lake haliwezi kushindwa.

<sup>279</sup> Kumbukeni, Yeye aliahidi, “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi.” Hawamwoni kwenye kinyang’anyiro cha hadhi usiku wa leo. Hawamwoni kwenye sinema. Hawamwoni katika makanisa haya baridi. Bali ninyi mnamwona. Yeye yupo hapa. Kumbukeni, Yeye aliahidi hilo, na Yeye yupo hapa kujibu maombi yako na kukupa shauku ya moyo wako.

Wekeaneni mikono na muombe.

<sup>280</sup> Bwana Yesu, naja, nikiukumbuka ya kwamba Wewe ulisema, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Nami ninaondolea mbali kila roho wa kutokuamini kutoka kwa kusanyiko hili, kutoka kwa watu hawa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.



*KUMKUMBUKA BWANA* SWA63-0122

(Remembering The Lord)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne jioni, tarehe 22 Januari, 1963, kwenye Southside Assembly Of God huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)